Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KWANZA

**Kikao cha Tatu - Tarehe 30 Desemba, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tisa na Nusu Alasiri)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samwel J. Sitta) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi kutoa taarifa kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alionyesha nia ya kuja kulihutubia Bunge hili kwa kuwa ni Bunge la Kwanza la Awamu hii na pia kulifungua. Shughuli hiyo ya Mheshimiwa Rais kulihutubia Bunge na kufanya ufunguzi rasmi itafanyika saa 10.00 jioni. Pamoja na wahudhuriaji wengine ambao wapo kwenye nafasi za wageni, kuna Marais Wastaafu ambao ingefaa na ingependeza wawemo ndani ya Bunge hili wakati Rais akilihutubia Bunge. Kwa hiyo, nitamwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atoe hoja ya kutengua Kanuni ya Bunge ili Bunge likubali kwamba Marais Wastaafu waingie Ukumbini na wakae pamoja na Wabunge. *(Makofi)*

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE ILI MARAIS WASTAAFU WAWEZE KUINGIA NA KUKAA BUNGENI

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 114 ya Kanuni za Bunge naomba kutoa hoja kwamba Viongozi Wastaafu wa nchi yetu waruhusiwe kuingia na kukaa ndani ya Ukumbi wa Bunge wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakapotoa hotuba ya kufungua rasmi Bunge jipya leo siku ya Ijumaa, tarehe 30 Desemba, 2005. Viongozi wahusika ni hawa wafuatao:-

- Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi - Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

- Mheshimiwa Benjamin William Mkapa - Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, kanuni husika inatenguliwa na Bunge hii ili kuwaruhusu Marais wetu wastaafu wakae pamoja nasi wakati Mheshimiwa Rais anazungumza na Bunge hili.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, itafaa kusitisha shughuli ili kuweza kumpokea Mheshimiwa Rais.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani ni vizuri niwasomee mtiririko wa matukio kabla sijasitisha shughuli za Bunge. Hivi punde nitasitisha shughuli za Bunge letu ili tuweze kutoka nje kumpokea Mheshimiwa Rais. Baada ya kumpokea, limeandaliwa gwaride maalum ambalo Waheshimiwa Wabunge mtaweza kushuhudia, ni nyuma ya Ofisi pale kuna eneo la wazi.

Mheshimiwa Rais akishakagua gwaride atarejea, tutampokea tutamuweka pahali ili Waheshimiwa Wabunge muweze kurejea ndani na kutulia. Baada ya hapo Mheshimiwa Spika ataongoza msafara wa Mheshimiwa Rais kuingia ndani ya Bunge ili Mheshimiwa Rais aweze kulihutubia Bunge.

Baada ya Mheshimiwa Rais kuongea na nimedokezwa itakuwa ni hotuba ya kama saa moja na dakika 15 ama 20, baada ya Mheshimiwa Rais kutoa hotuba, basi nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe *vote of thanks* kwa niaba ya Wabunge wote. Baada ya hapo, nitasitisha shughuli ili kumsindikiza Mheshimiwa Rais kutoka nje ya Ukumbi.

Sasa, pale nje kutakuwa na tukio la kupiga picha. Tutaomba Waheshimiwa Wabunge tuwe makundi mawili. Kwa sababu ya idadi yetu, haitawezekana kupiga picha ambayo nyuso zitaonekana sawasawa ikiwa ni picha moja kwa sisi sote 319. Kwa hiyo, tutapiga kwa makundi mawili. Kwa sasa hivi tunasema tu upande huu wa kulia wa Mheshimiwa Spika, utapiga kwanza, nadhani tutakavyochanganyika itakuwa vigumu hata hilo kuwezekana, lakini nadhani Katibu atatuelekeza ili iwezekane makundi mawili yapige picha.

Baada ya hapo tutamsindikiza Mheshimiwa Rais na ataondoka katika maeneo ya Bunge, kengele italia na Waheshimiwa Wabunge mtatazamiwa kurejea ili tufanye kazi ile ya uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika. Tutasubiri, matokeo yatatangazwa na baada ya hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atatoa hoja ya kuahirisha Bunge. Nitawahoji, mkiafiki basi Bunge litaahirishwa hadi tarehe itakayotajwa. Huo ndiyo mtiririko wa shughuli za leo. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge ili tuweze kutoka kuweza kumsubiri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kumlaki. Tuendelee na shughuli hizi.

*(Saa 9.37 Alasiri Bunge Lilifungwa ili Kwenda Kumpokea Mheshimiwa Rais)*

*(Hapa Marais Wastaafu Waliingia Bungeni na Kushangiliwa kwa Vifijo)*

*(Hapa Makamu wa Rais na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Waliingia Bungeni na Kushangiliwa kwa Vifijo)*

*(Hapa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa Aliingia Bungeni na Kushangiliwa kwa Vifijo)*

*(Saa 10.00 Bunge Lilirudia)*

*(Hapa Msafara wa Spika na Mheshimiwa Rais Uliingia Bungeni)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waheshimiwa Marais Wastaafu; Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania; Mheshimiwa Rais wa Zanzibar; Mheshimiwa Makamu wa Rais;

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuwa nimewataarifu awali, leo Rais wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete atalihutubia Bunge. Ni jambo la furaha na nadhani kwa niaba yenu kwa sababu ndiyo mara ya kwanza anakutana hapa na Bunge, nimpongeze sana kwa ushindi alioupata kwa niaba yenu. Sote tunamwombea afya njema, hekima, busara na subira ili aiendeleze nchi yetu tukishirikiana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, Wabunge wapo tayari kukusikiliza, karibu sana ulihutubie Bunge. *(Makofi)*

## UFUNGUZI RASMI WA BUNGE JIPYA

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kushukuru. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uhai na afya na ametukutanisha hapa leo. Ninamshukuru pia kwa kutuwezesha kufanya Uchaguzi Mkuu kwa amani, kwa utulivu na kwa heshima kubwa kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Nakishukuru sana Chama changu CCM, kwa heshima kubwa kilichonipa kwa kuniteua niwe mgombea wake wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru wananchi kwa kunipa mimi na Chama changu ushindi mkubwa sana. Shukrani zangu kwa Watanzania wenzangu, wana-CCM na wasiokuwa wana-CCM ni ahadi ya kuwatumikia kwa uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Nawashukuru watani zetu wa Kambi ya Upinzani kwanza, kwa ujasiri wao mkubwa wa kujitokeza kushindana na Chama cha Mapinduzi, maana kushindana na CCM siyo mchezo! Uchaguzi sasa umekwisha, naomba ndugu zangu tuungane, tuwe kitu kimoja, tujenge na kuendeleza nchi yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kumkubali mteuliwa wa CCM kwa nafasi ya Spika, Mheshimiwa Samwel John Sitta. Kadhalika, nawashukuru kwa kumkubali dada yangu Anna Semamba Makinda kuwa Naibu Spika. Ameweka historia ya Bunge letu kuwa na Naibu Spika mwanamke. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana pia kwa kunikubalia kwa uteuzi wa Ndugu Edward Ngoyai Lowassa kuwa Waziri Mkuu. Nimemteua Ndugu Lowassa si kwa sababu ya urafiki kama mtu mmoja alipojaribu kusema, lakini ni kwa sababu ya kutambua uwezo wake, uchapakazi wake na uimara wake katika kufuatilia mambo. Naomba mumpe Waziri Mkuu na Mawaziri na Naibu Mawaziri nitakaowateua hivi karibuni kutoka miongoni mwenu ushirikiano mkubwa. Wachangamsheni, lakini watendeeni haki na wapeni ushirikiano na heshima wanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu. Ninyi Waheshimiwa Wabunge ndiyo macho na ndiyo masikio ya wananchi. Mmeaminiwa na mmeheshimiwa na wananchi. Naomba kila siku mnapoingia au kutoka katika Bunge hili, mnapozungumza humu ndani au mnaposikiliza wengine wakizungumza, mnapokuwa macho au mnapofumba macho kutafakari hoja zinazoendelea; maana Mbunge hasinzii jamani, anafumba macho, anatafakari kwa kina yanayozungumzwa...*(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kila mara naomba mkumbuke imani na heshima kubwa mliyopewa na wananchi waliowachagua. Lakini msisahau pia mkawa mnasheherekea ushindi tu, lazima mkumbuke ipo siku ya kuulizwa na siku hiyo siyo ndefu sana, ni miaka mitano ijayo watakapokuja kukuuliza: "Umefanya nini ili tukupe tena ridhaa ya kuendelea?" Lakini suala baya zaidi "Ulikuwa wapi? Mwenzetu yalikukuta yapi hata leo ndiyo unarudi tena miaka mitano baadaye!" *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana wewe mwenyewe kwanza, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge; pili, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu. Umepata kazi ya heshima kubwa sana, yenye wajibu mkubwa sana. Una uwezo na uzoefu wa kuifanya kazi hiyo. Mimi sina shaka utaimudu vyema kabisa na utaliongoza Bunge hili kwa hekima na busara, ukiwatendea haki Wabunge wote, lakini pia ukiutendea haki upande wa Serikali yetu. Nakutakia kila la kheri, nakuhakikishia ushirikiano wangu kamili na wa Serikali yangu katika kufanikisha kazi zako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii pia kwa mara nyingine tena, nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Abeid Amani Karume kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar. Sikushangaa alipochaguliwa kwa sababu kuchaguliwa kwake ni matokeo ya kazi nzuri aliyoifanya katika miaka mitano aliyoiongoza Zanzibar. Ninamuhakikishia ushirikiano wangu na wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, navipongeza sana vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi yetu, kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa kisiwa cha amani na utulivu wakati wote wa mchakato wa uchaguzi.

Wameonyesha uaminifu kwa Taifa na uzalendo wa hali ya juu kabisa. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wameelimika na kufuatilia mchakato wote wa Uchaguzi Mkuu kutokana na kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Vyombo vya Habari. Nawashukuru na kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne ambayo nimepewa heshima ya kuiongoza inaanza wakati nchi ikiwa na hali nzuri kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mafanikio haya yametokana na uongozi imara na thabiti wa Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Napenda kuitumia fursa hii kumpongeza kwa dhati, kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanyia nchi yetu. Kwangu binafsi amekuwa Mwalimu, lakini amekuwa mwelekezaji mahiri ambaye amenijengea uwezo na dhamira ya kuendeleza kazi aliyoianza. Namtakia afya njema na maisha marefu yeye, Mama Mkapa na familia yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuzipongeza Tume ya Uchaguzi ya Taifa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kazi nzuri sana waliyofanya katika chaguzi zilizopita. Imethibitika kwamba uchaguzi wa mwaka huu umeendeshwa vizuri zaidi kuliko chaguzi zilizopita. Naomba waendelee kunoa uwezo wao maana Watanzania wa Bara na Zanzibar wanastahili uchaguzi mzuri na wanastahili uchaguzi wa haki. Kadhalika, tunao wajibu wa kihistoria sisi Tanzania kwa kuwa mfano bora Barani Afrika na hata kwingineko. Nilipata bahati ya kuzungumza na baadhi ya waangalizi wa Kimataifa, wameshangaa sana jinsi uchaguzi ulivyoendeshwa vizuri na taratibu nzuri zilizokuwepo na wameahidi zingefaa zisambazwe ili na nchi nyingine ziige jinsi Tanzania ilivyoendesha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kimerejeshwa madarakani kwa kura halali za wananchi zilizotupa idhini ya kuongoza na kutawala, tena idhini kubwa isiyokuwa na mashaka hata kidogo. Hatutaona aibu kuitumia idhini hiyo kupitia Bunge hili kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kama mwana-CCM nafurahia sana ushindi wetu, lakini nikiwa Rais napenda niwahakikishie wenzetu wa upinzani kuwa sina nia, CCM haina nia wala sera ya kuua Vyama vya Upinzani. Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza kwa dhati kabisa Mfumo wa Siasa ya Demokrasia ya Vyama Vingi. Ushauri wangu tu kwa Vyama vya Upinzani ni kuacha kuwa wepesi wa kutafuta mchawi kila wanaposhindwa uchaguzi. Lakini si vibaya maana ukiwa mkweli wakati mwingine unaweza kujua kwamba mchawi ni wewe mwenyewe. Badala yake nawaomba wajiulize kwa nini Watanzania wamewakataa kiasi hicho! Nina uhakika watapata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi yetu sasa ni ya Demokrasia ya Vyama Vingi, lakini ni wazi bado utamaduni wa mfumo huu wa siasa ni mchanga na kwa ujumla haujaimarika vya kutosha. Tutajitahidi kujenga utaratibu na msingi wa mahusiano mema zaidi baina ya Vyama vya Siasa nchini Tanzania. Naamini wakati umefika kama alivyowahi kusema Rais Mkapa wakati ule kuwa: “Tuwe na maadili yatakayotawala

shughuli za siasa ambayo hayategemei hiari ya Kiongozi wa Siasa aliyepo madarakani, bali yanakuwa ni maadili na miiko ya lazima yanayobana kila Chama cha Siasa, Wanachama wake, Viongozi wake, kikiwemo na Chama Tawala." *(Makofi)*

Ndugu zangu, wenzetu wamefanya hivi na imesaidia. Tusipofanya hivi na dalili zimeanza kuonekana, kwamba wanaweza kujitokeza watu wakavuruga nchi yetu kwa kisingizio cha uhuru wa kisiasa. Uhuru bila mipaka ni fujo na siwezi kukubali nchi mliyonikabidhi kuiongoza itawaliwe kwa fujo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yameanza kujitokeza mawazo kuwa uongozi unaweza kununuliwa kwa fedha. Tusipokuwa waangalifu nchi yetu inaweza kuwekwa rehani kwa watu wenye fedha za kununua uongozi au wanaoweza kupata fedha za kufanya hivyo, maana anaweza kufadhiliwa na mtu ili anunue uongozi. Ni kweli kwamba fedha ni nyenzo mojawapo muhimu katika kufanikisha uchaguzi, lakini fedha kutumika kununua ushindi si jambo halali. Ni vyema sasa tulizungumze na tulishughulikie suala hili. Naomba wenzangu kama ni mjadala wa Kitaifa tufanye na hatimaye tuelewane kuhusu utaratibu halali ulio wazi wa Chama au Mgombea kutafuta fedha za uchaguzi na utaratibu halali ulio wazi wa chama au mgombea kutumia fedha hizo, maana hii ya kupata fedha mivunguni hii, unakwenda tu ghafla Mbunge, ghafla umekuwa mkubwa, lakini kuna watu waliokufikisha pale, au unatumia utajiri wako tu kufika hapo! Utaratibu tutakaokubaliana kwa mapendekezo yangu uwe ni sehemu ya maadili ya uchaguzi katika chaguzi za Serikali, lakini pia katika chaguzi ndani ya Vyama vya Siasa. Katika mjadala huo suala la takrima nalo tulijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tupate uhuru, kila Awamu ya Uongozi wa Taifa imekuwa na jukumu lake au kwa lile nililokuwa nazungumza kwa Kiingereza, nataka kusema ni *campaign finance.* Lazima tuwe na *ethics* za *campaign finance.* Nirudie, nasema hivi, kila awamu imekuwa na majukumu yake ya msingi. Awamu ya Kwanza iliunda na kujenga Taifa la Tanzania. Mzee Nyerere aliunda Taifa la Tanganyika, Mzee Karume aliunda Taifa la Zanzibar.

Wakoloni hawakujenga hisia za utaifa, maana mkakati wao wa kututawala ulikuwa ni kutudhoofisha, kutugawa ili tutawalike kwa urahisi. Mwalimu Nyerere hakurithishwa Taifa na Wakoloni, alirithishwa mkusanyiko wa makabila mbalimbali, mkusanyiko wa watu wa dini mbalimbali na mkusanyiko wa watu wa rangi mbalimbali, lakini alitambua kuwa hata kama uchumi wa Tanzania ungekua kwa kasi kubwa kiasi gani, iwapo hakuna msingi imara na hisia ya dhati ya utaifa, baada ya muda mfupi Taifa hilo litasambaratika na uchumi huo utakuwa hauna maana tena. Itakuwa labda *bubble gum economy* au itakuwa *house of cats.* Ukibonyeza zinaanguka.

Kwa kushirikiana na Hayati Rais Abeid Amani Karume wakatujengea Taifa la Tanzania lenye umoja, pamoja na kuwa ni Taifa la makabila 120 wa rangi mbalimbali, naona na Hoogan yupo Singasinga, Aziza Mwarabu yumo, Wanyamwezi wapo, makabila mbalimbali, dini mbalimbali, lakini amefanya jitihada ya kujenga Taifa moja. Mwalimu alirithi Taifa maskini sana, aliongoza vita dhidi ya ujinga, umaskini na maradhi, kwa jitihada zake na kwa kiasi chake cha uwezo. Mtandao mkubwa wa huduma

za jamii, tunaojivunia leo ulianza na falsafa ya maendeleo ya Baba wa Taifa. *(Makofi/Kicheko)*

Wengi wetu tuliomo humu ndani hasa wa makamo yangu tusingesoma hata kufika hapa tulipo kama sio kuona mbali na sera nzuri za Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere. Tutamshukuru yeye na Mzee Karume daima.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Pili chini ya Mzee wetu Alhaj Ali Hassan Mwinyi, maarufu kwa Mzee Rukhsa, lakini rukhsa tunayoizungumza ni kwamba Mzee Mwinyi alifungua milango na kupanua uwanja wa ushiriki wa wananchi kwenye uchumi wa kisasa. Lakini pia alifungua milango ya kushiriki wananchi kwenye siasa. Ndiyo maana leo Bunge letu lina Kambi ya Upinzani. Ni rukhsa ya Mzee Mwinyi. Mzee Mwinyi ni Muasisi wa Mageuzi ya Kisiasa na Kiuchumi nchini Tanzania. Alimaliza uhaba wa bidhaa na baadhi ya huduma muhimu zilizodhalilisha maisha ya Watanzania. Alipanua sana mipaka ya uhuru wa raia katika maisha yao ya uchumi na kisiasa. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini nakumbuka siku moja Mzee Mwinyi alisema, "Awamu yake aliifananisha na wakati ambapo mtu anafungua madirisha ya nyumba ili hewa safi iingie ndani. Lakini akasema ukifungua madirisha, ujue inzi wanaingia, mbu wanaingia na wadudu wengine pia usiowataka wanaingia humo ndani". *(Makofi/Kicheko)*

Hapo ndipo Awamu ya Tatu ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, aliyenitangua ilipoanzia. Kazi yake ya kwanza ilikuwa kushughulikia mbu, inzi na wadudu hao waliojipenyeza. Rais Mkapa alifanya kazi kubwa ya kurejesha nidhamu kwenye ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali. Lakini jinsi ya nidhamu kwa ujumla katika utendaji wa Serikali. Alipiga vita rushwa kwa nguvu zake zote, lakini ndani ya mfumo wa utawala wa sheria, alirejesha mahusiano mazuri na Wahisani wetu na washirika wetu wa maendeleo.*(Makofi)*

Aliweka mazingira mazuri kwa uwekezaji na ukuaji wa uchumi, aliimarisha misingi ya uchumi Mkuu. Bei za kuruka na fedha za soksi zikapotea. Matokeo yake wakasema Mzee ameleta Ukapa. Lakini wale waliopata fedha kwa taratibu zisizokuwa halali ndiyo waliliona tatizo hili. Lakini ameweka misingi imara ya kuwezesha wananchi kujiendeleza pia kupitia miradi ya TASAF na sasa MKURABITA chini ya mfumo wa mwavuli wa MKUKUTA. *(Makofi/Kicheko)*

Alikarabati na kupanua sana miundombinu ya elimu, afya, maji, umeme na kama tunavyojua, sote tujuavyo, kazi kubwa ya ujenzi wa barabara na madaraja imefanywa na inaendelea. Kutokana na juhudi za Rais Mkapa ndani ya nchi na Kimataifa, Serikali ya Awamu ya Nne, inaanza bila mzigo wa madeni usiobebeka kama alivyoanza yeye.

Siku ambayo alikuwa ananikabidhi madaraka, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* lilitangaza rasmi kuwa Tanzania ni moja ya nchi ambazo uamuzi wa mwisho umefikiwa wa kutufutia madeni ya nje. Tumshukuru kiasi gani? Tunaanza mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, sasa ni wakati wa kubainisha majukumu ya msingi ya Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imetamka bayana majukumu mawili ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kwanza, kufanya jitihada za kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na uchumi tegemezi na kuingiza nchi yetu katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. *(Makofi)*

Pili, kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kutokomeza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu haya ya msingi, mbinu na mikakati mbalimbali ya kuyatekeleza, Watanzania watazamie mambo kumi yafuatayo katika miaka mitano ijayo:-

Kwanza, Serikali ya Awamu ya Nne, itahakikisha kuwa amani, utulivu na umoja wa nchi yetu na watu wake vinadumishwa. *(Makofi)*

Pili, Serikali ya Awamu ya Nne, itadumisha na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza mpaka sasa. *(Makofi)*

Tatu, Serikali ya Awamu ya Nne, itaendeleza vita dhidi ya umaskini, ujinga na maradhi tena tutafanya hivyo kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Nne, Serikali ya Awamu ya Nne, itatimiza ipasavyo wajibu wake wa utawala na maendeleo na itaendesha dola kwa misingi ya utawala bora na uwajibikaji na uwazi. Utawala wa Sheria, unaoheshimu na kulinda haki za binadamu na haki za raia wote. Serikali ya Awamu ya Nne, itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa bila ya woga wala kuoneana muhali. *(Makofi)*

Tano, Serikali ya Awamu ya Nne, itaimarisha uwezo wake wa kulinda maisha na mali ya raia wake. Tutapambana na uhalifu bila aibu, bila uwoga, uhalifu wa kila aina na majambazi hayataachwa yatambe yatakavyo. *(Makofi)*

Sita, Serikali ya Awamu ya Nne, itahakikisha kuwa mipaka ya nchi yetu iko salama. Hatutamruhusu mtu au nchi au watu kuchezea mipaka ya nchi yetu na uhuru wetu. *(Makofi)*

Saba, Serikali ya Awamu ya Nne, itafanya kila liwezelo kuhakikisha kuwa Tanzania ina mahusiano mazuri na mataifa yote duniani pamoja na mashirika ya kimataifa na kikanda. *(Makofi)*

Nane, Serikali ya Awamu ya Nne, itajali sana maslahi na mahitaji ya makundi maalum katika jamii kama vile wanawake, vijana, watoto, wazee, walemavu na yatima. *(Makofi)*

Tisa, Serikali ya Awamu ya Nne, itaongoza mapambano mapya ya kuhifadhi mazingira ili vizazi vijavyo virithi nchi nzuri na wawe na misingi mizuri na imara ya maendeleo endelevu; na *(Makofi)*

Kumi, Serikali ya Awamu ya Nne, itaendeleza michezo na shughuli za utamaduni na burudani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umoja wa kitaifa wa Tanzania ni moja ya jambo ambalo tumeahidi tutalisimamia, ni mhimili Mkuu wa amani na utulivu. Watanzania wanaenzi sana umoja wao na amani yao. Naamini ndio maana wameacha kuvipigia kura Vyama vinavyohusishwa na vurugu na/au Vyama ambavyo msimamo wao kuhusu umoja na Muungano unatiliwa mashaka.

Umoja wa Kitaifa wa Tanzania, una sura mbili. Upande mmoja ni Muungano wetu, yaani umoja wa nchi zetu mbili huru zilizoungana kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muungano wetu una miaka 41 sasa, ni wa pekee Afrika. Pamoja na kuwepo matatizo ya hapa na pale, Muungano bado ni imara na ni wa kujivunia. *(Makofi)*

Upande wa pili wa umoja wa kitaifa ni umoja wa raia wenyewe wanaojihisi wote ni Watanzania kwanza, bila kujali tofauti zao za makabila, dini, rangi, jinsia au maeneo wanayotoka.

Kazi mojawapo ya msingi ya Serikali nitakayoiunda ni kulinda, kudumisha, kuendeleza na kuimarisha Muungano wetu. Tunakusudia tufanye hivyo kwa kufanya mambo yafuatavyo:-

Kwanza, kwa ujumla, tutakuwa makini na wepesi katika kushughulikia matatizo ya Muungano. Tutayazungumza kwa uwazi na kuchukua hatua muafaka kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Pili, nakusudia kumpunguzia Makamu wa Rais mzigo wa shughuli za kuondoa umaskini ili apate muda wa kutosha wa kushughulikia masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Tatu, nitaimarisha taratibu zilizopo, zilizoanzishwa na Serikali zilizopita za kujadili, kuainisha na kutatua matatizo ya Muungano. *(Makofi)*

Nne, tunakusudia kuongeza mchango wa Serikali ya Muungano, katika maendeleo ya uchumi na kijamii ya Zanzibar, bila kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo ambayo si ya Muungano. Lakini naamini uchumi wa Muungano ambao ni mkubwa zaidi nao unao wajibu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nimesema umoja wa Tanzania unahusu umoja wa wananchi, miongoni mwao wananchi wanaotokana na makabila zaidi ya 120 na wa maeneo, rangi na dini mbalimbali. Lakini Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere aliwafanya Taifa moja, lenye umoja wa kitaifa unaopigiwa mfano kote Barani Afrika na duniani. Hili ni jambo jema, jambo la kujivunia na jambo la kudumishwa na kuendelezwa kwa nguvu na bidii zetu zote.

Ipo hofu ya kweli, miongoni mwa Watanzania kuwa bado wapo miongoni mwetu watu wanaotaka kuturudisha tulikotoka, tuanze tena kuulizana wewe kabila gani? Ndipo tufanye uamuzi wa kusaidiana. Tuanze tena kuulizana na kubaguana kwa misingi ya dini; Wewe dini gani? Na kubaguana kwa misingi ya kabila zetu, tuanze tena kutazamana kwa rangi zetu na maeneo tunayotoka.

Nawasihi sana ndugu zangu Watanzania wenzangu tunaowania uongozi wa ngazi zote zile tangu chini mpaka juu, uongozi wa Kiserikali, uongozi wa kisiasa ndani ya Vyama vyetu au uongozi wa dini, tusitumie ubaguzi wa aina yoyote ile. Naomba kwa pamoja tusiwavumilie, wala tusiwaache watu wa aina hiyo waigawe nchi yetu. Hawatavumiliwa na hawataachwa waigawe nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema jambo sasa hivi, lakini naomba mnielewe nia yangu nzuri sana. Nachukua uongozi wa Taifa nikiwa nasononeshwa sana na mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba na pengine kati ya Pemba na sehemu nyingine za Jamhuri yetu. Matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, umedhihirisha mpasuko huo ambao naamini chanzo chake ni historia. Lakini historia hiyo ya wanadamu, wanadamu hawalazimiki kuwa wafungwa wa historia yao isiyoleta tija na maslahi. Natoa mifano, msinielewe vibaya. Natoa mifano ya hali ninayoiona. Iweje leo Wapemba ambao ni hodari wa kutumia fursa ya Muungano wetu na kuishi na kufanya biashara na kuwekeza katika pembe zote za Jamhuri yetu wawe hao hao wanaoonekana kama wanajitenga kisiasa kwa kiwango tunachokishuhudia kwenye Uchaguzi Mkuu? Iweje leo wana ndugu, Wapemba na Waunguja waishi kwenye mazingira ya uhasama?

Ndugu zangu, wakati umefika wa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mpasuko huo. Nategemea kupata ushirikiano mzuri kutoka kwa wanasiasa wa pande zote wa Zanzibar. Nimeanza kwa kuomba radhi, naomba mnielewe dhamira yangu. Natambua sana kwamba uamuzi wa mwisho kuhusu hatma ya kisiasa na kiutawala ya Zanzibar ni ya Wazanzibari wenyewe. Lakini Jamhuri yetu ni moja, nchi yetu ni moja, yanayotokea Zanzibar yanatugusa sote. Pengine leo ni zaidi kuliko ilivyokuwa katika historia wakati ulipokuwepo msemo kuwa zumari likipigwa Zanzibar wanacheza mpaka Bara. Hivyo basi, nitakuwa tayari kuanzisha, kuwezesha na kusaidia mjadala mpana juu ya mustakabali wa kisiasa Zanzibar.

Naamini kuwa kuendeleza pale utekelezaji wa muafaka ulipoishia kabla ya uchaguzi, kutasaidia mikakati na mbinu nyingine mpya. Najua si kazi rahisi, lakini nchi hii ni yetu sote. Nakusudia kufanya kila lililo ndani ya uwezo wangu ili siku awamu yangu ya uongozi wa Jamhuri yetu ikifika ukingoni nisiiache hali hii ya mpasuko wa

kisiasa kama nilivyoikuta. Kwa maana nchi moja hakuna anayeishi Zanzibar pekee yake tu. *(Makofi)*

Nilikwenda Mpanda, nikamkuta yuko Mpemba pale kwenye biashara ya dhahabu. Ukienda kwangu Bagamoyo pale wako wengi tu, wameoa sana watu maarufu kwa Wakojani, kila anayetoka huko awe Muunguja awe nani bora amekuja kwa kuvua anaitwa Mkojani kwa Bagamoyo. *(Kicheko)*

Ndugu zangu, zamani kulikuwa na msemo unaosema, Zumari likipigwa Zanzibar wanacheza kwenye Maziwa Makuu, *(they pipe in Zanzibar, they dance in the great lakes)*. Kwa sababu ya umoja wa nchi yetu sasa ni zaidi ya hiyo. Zumari likipigwa Kisiwa Panza, wa Kondoa anacheza. Zumari likipigwa Kizimkazi wa Mlingotini, kwa sababu nchi yetu ni moja, lakini pia hata Zumari la Mtendeni utalikuta na Bagamoyo lipo. Tunasema, hivi ndivyo tulivyo. Nitakuwa tayari kuanzisha, kuwezesha, kusaidia mjadala mpana zaidi juu mustakabali wa kisiasa sasa. *(Makofi)*

Najua muafaka ulisaidia, lakini fikra yangu ni zaidi ya muafaka. *Let engage ourselves on serious debate* ya matatizo yetu ya masuala yetu tuyatafutie majawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, inakusudia miongoni mwa mambo mengine kushughulikia suala la kuimarisha utaifa wetu kwa kufanya mambo kumi kadhaa yafuatayo:-

Nalizungumza hili kwa sababu kwenye suala la utaifa sipendi watu *to take for granted* mambo, tusipoendelea kulishughulikia unaweza kukuta kwamba Taifa linamomonyoka bila ya nyie kujua. Kuna siku mnaweza mkajikuta mmekuwa Wakwere tu, mmekuwa Waislamu tu, Walokole tu, Wakatoliki tu peke yake, mmekuwa Waha pekee.

Kwanza, kwa kutumia mfumo wa elimu kujenga na kuimarisha umoja wa kitaifa ikiwemo Shule za Sekondari za Kitaifa, kutenga Shule maalum za Serikali za Kitaifa zitakazochanganya kwa makusudi wanafunzi wenye vipaji mbalimbali kutoka pembe zote za nchi.

Katika mazingira ya sasa haya ya kuongezeka Sekondari za Kutwa za kila Kata, mnaweza mkaishi tukafika mahali ikawa mtoto hata kwenye Wilaya hajui kwamba kuna sehemu nyingine zaidi ya pale alipo yeye. *(Makofi)*

Mimi nilipokuwa mdogo, tupo Shule ya Msingi pale Wakwere watupu tunazungumza Kikwere na ukimwona mtu anakuja hajui Kikwere, unamshangaa!! Wewe unadhani dunia yote hii kila mtu anazungumza Kikwere tu. *(Makofi/Kicheko)*

Nilipokwenda Sekondari, ndiyo sasa nikaanza kukutana na watu, alaah, kumbe na huyu anatoka Bukoba, kumbe na huyu anatoka Moshi, ndiyo unaanza kuiona tofauti hiyo. Lakini ndugu zangu hatusemi Shule zote tutazifanyia hivyo, lakini *at least* tuwe na

baadhi ya Shule hata kama ni moja kwenye kila Mkoa au moja katika kila Wilaya ziwe zinatuchanganya hivyo ili tuzidi kujenga ushirikiano. *(Makofi)*

Pili, tufikirie kuiandaa mitaala ya somo la uraia itakayopanda mbegu za uzalendo na umoja wa kitaifa katika ngazi zote za ekimu. *(Makofi)*

Tatu, kuzipa changamoto Shule za Mashirika ya Dini isipokuwa Seminari kupokea wanafunzi wa dini zote. Kwa Seminari hapana. Kama iko Seminari ya Ununio ya Waislam huwezi ukasema na John naye akasome pale, maana yanayofundishwa pale, John hayamfai. Lakini iko Seminari ya Kipalapala huwezi ukasema na Rashid aende pale.

Lakini zile nyingine tunazozianzisha za Mashirika ya Dini, tunataka kujenga msingi wa Taifa kwa sababu ukianza tu ku-*concentrate* kufundisha watu wa dini yako tu kwenye Shule yako, unapanda mzizi wa kuligawa Taifa mbele ya safari. *(Makofi)*

Nne, kuendeleza kazi nzuri iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu ya kufufua Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Tano, kujenga muafaka baina ya vyama na makundi ya kijamii juu ya utambuzi wa heshima, tunu za Taifa kama vile haki, usawa, umoja na mshikamano. Hapa nazungumzia kitu gani? Wenzetu wamefika mahali ambapo kuna vitu, ni kama vile ni miiko, huwezi ukaigusa na anayegusa ile anawajibishwa wakati huo huo. Lazima tufike mahali tukubaliane baadhi ya vitu kwa sababu wako watu, ni *reckless* anaweza tu akaanza kuhutubia tu mimi siwataki Wazanzibar, anapanda jukwani Ukumbi wa Habari Maelezo na watu wanaona mazungumzo ya kawaida tu.

Kuna mtu anaweza akachagua tu iko siku akaamua kwamba hawataki Waislam tu akiwaona anasikia kichefuchefu. Hatuwezi kukubaliana na haya. Ama yeye Muislam anawachukia Wakristo, lakini nchi hii moja.

Wakati mmoja nilikuwa Marekani, maana Vyombo vya Habari si ndiyo vyenye uhuru mkubwa. Kulikuwa na Mtangazaji mmoja wa Redio ya Marekani wa mchezo wa *American Football,* alikuwa Mzungu huyu, anatoa mfano wa beki wa timu moja mweusi anasema yule bwana mpira wake mdogo wanampenda sijui kwa sababu ni mweusi!

Hili lilitosha kufukuzwa kazi kwenye Shirika lake. Kwamba hawakumvumilia tena, akaambiwa acha kazi, ondoka! Sasa ni lazima tufike hapo kwa sababu hivi ni vitu ambavyo tukiviachia vinamong'onyoa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sita, kutumia michezo, nyimbo, sanaa, kuimarisha hisia za utaifa na kujenga uzalendo na kuipenda nchi yetu. *(Makofi)*

Saba, kueneza na kuruhusu matumizi ya alama za kitaifa kama mambo ya kila raia kujivuna na kuyaheshimu sana. Maana unaweza kumwona mtu moyo wake wa uzalendo umempanda amefunga skafu ya bendera ya Taifa. Taratibu zetu hapa, huyu anatakiwa akamatwe ashitakiwe kwamba amedhalilisha bendera. Amependezwa sana, ameamua kushona shati la bendera ya Taifa, anaonekana amefanya kosa kubwa sana.

Mimi nasema hivi ni viashirio tu vya utendaji, vinasaidia kujenga uzalendo. Sasa vitu kama hivi tukae tujadiliane tuone itatusaidia kidogo kujenga vyema utaifa wetu. *(Makofi)*

Nane, kujenga na kuimarisha mahusiano kati ya dini, vyama vya siasa na makundi mbalimbali ya kijamii. Siasa siyo uhasama! Kuna mtu ukimweka CCM haoni raha, lakini akikaa CHADEMA ni raha mustarehe anajisikia roho yake. Mwache aende CHADEMA. Sasa tatizo ninaloliona mimi ni kwamba tunageuza siasa uhasama, tunapigana mawe, tunatukanana, haya ndiyo nasema ndugu zangu yanazidi tu kutufikisha mahali tunapoteza dira ya Taifa. *(Makofi)*

Sasa tufanye jitihada, Rais Mkapa alifanya jitihada kubwa ya Mikutano ya Vyama, mimi makusudio yangu tuna-*institutionalize* mazungumzo haya. Lakini pia kwa kulisisitiza hili hapa, katika Ofisi yangu, Ofisi ya Rais nakusudia tuwe na Waziri atakayekuwa anashughulikia Mahusiano ya Vyama na Mahusiano ya Jamii. Sasa hivi nafanya kupitia Washauri na Wasaidizi pengine tupate *stature* kubwa zaidi ya Waziri ili aweze kuwa na nguvu kubwa zaidi ya mawasiliano na Vyama.

Lakini kumi, kujenga utaratibu wa mazungumzo ili kutatua mapema migogoro katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo sababu kwa nini nchi yetu imekuwa kwa kiwango kikubwa kisiwa cha amani na utulivu katika bahari iliyotibuka. Mojawapo ya sababu hizo kama nilivyosema ni sera ambazo kwa makusudi kabisa zilijenga hisia za umoja, hazikuwabagua wala kuwanyima haki Watanzania kwa sababu ya dini, rangi, kabila na jinsia zao.

Tunakusudia sera hizo tuziendeleze na ninawatarajia watakuwa katika Serikali kwa maana Baraza la Mawaziri kamwe wasiwabague wananchi kwa sababu yoyote ile na wawe ni watetezi thabiti wa haki za raia na haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali nitakayoiongoza itakuwa inazingatia na kuendeshwa kwa misingi ya utawala bora, uwazi na uwajibikaji. Tutaheshimu utawala wa sheria na tutazingatia na kuheshimu mgawanyo wa madaraka kati ya mihimili mikuu ya dola, yaani Utawala, Bunge na Mahakama. Tutaheshimu uhuru wa Mahakama, tutaheshimu uhuru wa Bunge, lakini pia tutatimiza wajibu wetu ipasavyo wa kuwezesha mihimili hiyo kufanya kazi zake kama inavyotazamiwa. Pamoja na uhuru wenu lakini fedha yenu inatoka kwetu. Tunachoahidi ni kwamba wajibu huo sisi tutautimiza, hatutawaingilia kwenye mambo yenu. *(Makofi)*

Serikali ya Awamu ya Nne itazidi kuimarisha utendaji Serikalini na kupambana na maovu katika jamii bila woga wala kuona haya. Tutaongeza kasi ya kupambana na rushwa, tutaifanya kisayansi kwa kushambulia kiini chake na kuziba mianya yake. Rais Mkapa katika Tume ya Mheshimiwa Warioba, amefanya jitihada kubwa ya kuziba mianya. Tutafanya tathmini tumefikia wapi ili twende mbele zaidi. Tutajitahidi kuongeza na kuboresha mishahara na maslahi ya watumishi wa umma ili kupunguza

vishawishi vya rushwa. Hatuna uwezo usiokuwa na ukomo, lakini tutafanya jitihada hali iwe bora kila wakati. *(Makofi)*

Tutaendelea pia kuongeza uwazi katika maamuzi ya Serikali hasa katika manunuzi na miakataba. Tutaimarisha uwezo wa kifedha na kiutendaji wa taasisi zilizoko mstari wa mbele kwenye vita dhidi ya rushwa, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Jeshi la Polisi na Mahakama. Lakini yote hayo ni bure iwapo wananchi hawatajitokeza kusaidia vyombo hivyo. Naomba ushirikiano huo kutoka kwa wananchi. *(Makofi)*

Lakini katika harakati za kupambana na rushwa, yapo mambo mawili mengine ambayo tutayaangalia kwa karibu. La kwanza ni mikataba. Tutaangalia upya taratibu za mikataba mbalimbali inayoingiwa na Serikali, Mashirika ya Umma na Idara zinazojitegemea kwa nia ya kuongeza uwazi na uwajibikaji. Mikataba ni mwanya mkubwa wa rushwa, hasa zile rushwa nene nene, rushwa za wanaotafuta utajiri. *(Makofi)*

Kadhalika, hatuna budi kuchukua hatua thabiti za kuzuia Watumishi wa Umma kutumia nafasi zao kujitajirisha na kujilimbikizia mali. Sisemi kwamba ni haramu mtu kuwa tajiri au kuwa na mali, hapana. Ninachosema mimi kuwa ni haramu ni kutumia nafasi ya Utumishi na Uongozi wa Umma kujipatia manufaa, kujitajirisha au kujilimbikizia mali. Ni jambo jema kwani sera yetu inalenga kuinua hali ya maisha ya watu kwa kupambana na umaskini wa kipato. Ninachosema mimi, ni kwamba haramu ni kutumia nafasi yako ya Utumishi au Uongozi wa Umma kujipatia manufaa ya kujitajirisha au kujilimbikizia mali. *(Makofi)*

Jambo hili ndilo linalokera sana Watanzania wanapomwona mtu ambaye hana chochote lakini miezi michache tu baada ya kupata cheo anakuwa tajiri mkubwa. Keshakuwa Mbunge au Waziri, Katibu Mkuu au Mkurugenzi au Mkuu wa Idara, mwaka haujapita ana majumba ya fahari, madaladala msururu ana *taxi* bubu, anaishi maisha ya kifahari yasiyoelezeka, haya ndiyo mambo ambayo wananchi wanahoji. Wanayo haki kuhoji na wanastahili kupata majibu kwa wanayohoji. Ndugu zangu, naomba tuwe waadilifu na waaminifu, tusilaumiane mbele ya safari. *(Makofi)*

Kwa vyovyote, inatia shaka ya kuwepo mazingira ya rushwa. Serikali ya Awamu ya Nne haina budi ichukie tabia hiyo na kila mmoja wetu awe askari wa kupambana nayo. Naiomba Tume ya Maadili ya Viongozi isione haya kutuuliza jinsi tulivyozipata mali zetu ambazo tunasema tunazo. Tumesema unaweza kuzipata halali tu, *don't worry about it,* sisemi kwamba wafanye *harrassing*. Lakini nasema tukifanya hivi itatusaidia mbele ya macho ya watu. Mbele ya macho ya watu ,viongozi wanaonekana kwamba ukipata nafasi ya uongozi, basi umeukata. Kwa lugha ya Dar es Salaam pale, ni kwamba sasa wewe shida zako zimekuishia na umaskini umeupa kisogo.

Ndugu zangu, naomba Tume itusaidie na itawasaidia kujenga uwezo huo kama hilo ndiyo tatizo lao. Tusingoje mpaka mtu aje kulalamika. Nitawasaidia kujenga uwezo wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, dhana ya utawala bora ni pana sana, ni zaidi ya vita dhidi ya rushwa. Serikali ya Awamu ya Nne itashughulikia maeneo yote ya utawala bora. Tutatimiza utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa ustadi, kwa haraka na kwa ufanisi. Tunataka Watendaji wa Serikali wawe waadilifu, wawe ni watu wanaowajibika, wawe na ari na moyo na msimamo wa dhati kuhusu utumishi wa umma na huduma bora kwa wananchi. Tabia ya njoo kesho na nenda rudi ndugu zangu tuiache. Linalowezekana leo lisingoje kesho. Kwa nini iwe kila siku njoo tu kesho? Hakuna lisilowezekana. Napenda huo uwe moyo wa utendaji Serikalini sisemi kwamba hali ni mbaya lakini hii iwe msisitizo na *spirit* yetu. (Makofi).

Nitataka watakaokuwa kwenye Serikali ya Awamu ya Nne, wajijengee tabia ya mara kwa mara wao wenyewe kujiuliza iwapo kwa maamuzi yao, kwa vitendo vyao na kwa tabia zao wanajenga au wanabomoa heshima ya Serikali machoni pa wananchi.

Natambua tatizo na malalamiko ya watumishi wa umma kuhusu mishahara na maslahi yao. Nimesema tutaliangalia. Tutalishughulikia. Rais Mkapa wakati wake alikusudia kuliangalia, kuliundia Tume na kuboresha maslahi ya umma. Mimi ahadi yangu niliyoitoa kwa Watanzania ni kwamba yale ambayo Rais Mkapa alikusudia kuyafanya lakini hakuyamalizia mie sasa ndiyo niko hapa kuyafanya. Tume hiyo tutaiunda mapema iwezekanavyo ila naomba niwatahadharishe tusiwe na matumaini makubwa mno, kwa sababu bado siyo mkubwa sana. Lakini tutafanya kinachowezekana kadri ya uwezo wa Serikali unavyojengeka ili mwaka hadi mwaka watu waanze kuona tofauti ya walivyokuwa kabla.

Nakusudia mapema iwezekanavyo niteue Tume ya Kuboresha Maslahi ya Watumishi wa Umma, lengo ni kuwa na mkakati wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa kuongeza mishshara na kuboresha maslahi yao. Hatua hizo zitawawezesha wafanyakazi wa umma kumudu maisha yao na kupunguza manung'uniko na milipuko ya migogoro.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utoaji haki, kwa kuongeza idadi ya watumishi, kuwaendeleza kitaaluma, kukarabati majengo yaliyopo, kujenga mapya na kupeleka huduma za utoaji haki zaidi kwa wananchi. Sisemi tutafanya sisi, lakini tutaiwezesha Mahakama yafanywe hayo maana yake tukifanya sisi tutakuwa tumeingilia uhuru wa Mahakama jitihada kubwa zimefanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu kuimarisha Mahakama na kuanzisha vitengo maalum vya Mahakama Kuu hususan, Mahakama ya Ardhi na Mahakama ya Biashara.

Serikali nitakayoiunda, pamoja na kuheshimu uhuru wa Mahakama, itatimiza ipasavyo wajibu wake na kuimarisha miundombinu ya kutoa haki kwa kuongeza idadi ya watumishi, kuwaendeleza kitaaluma, kukarabati majengo yaliyopo na kujenga mapya na kupeleka huduma za utoaji haki karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kusimamia vizuri mapato na matumizi ya Serikali nayo ni sehemu ya utawala bora. Isitoshe, utekelezaji mzuri wa jukumu hilo ndio unaipa Serikali uwezo wa kutekeleza mengine yote inayopaswa au inayokusudia kuyatekeleza. Serikali

ya Awamu ya Tatu, chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, iliongeza mapato ya Serikali mara tano sambamba na kuweka mfumo mpya na wa kisasa wa kudhibiti matumizi na kuongeza uwazi katika bajeti ya Serikali. Hatutalegeza kamba hata kidogo.

Ahadi tunayoitoa kwa Watanzania ni kwamba, hatutavumilia wanaokwepa kodi stahiki za Serikali, hatutawavumilia wabadhirifu wa mali za umma, Sheria ya Fedha na Sheria ya Manunuzi ya Umma kuhakikisha kwamba zinafuatwa ipasavyo. Watakaokiuka wachukuliwe hatua za nidhamu na zichukuliwe wakati huo huo. *(Makofi)*

Unajua wakati mwingine vinashangaza! Zamani *Auditor* akienda kukagua, akikuta fedha zimeibiwa, huwa anampeleka mtu Polisi. Sijui wanafanya hivyo? Maana naona ripoti nyingi zinakuja kwenye taarifa yako ya Bunge hapa. Sasa baada ya hapo Bunge linafanya nini? Mtu akiiba mchukueni mpelekeni Polisi atakwenda kujibu na Polisi. *(Makofi)*

Sasa ukingojea mpaka utakapoileta kwenye Kamati, wakati ule Kamati ilikuwa ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na wakati mwingine Kamati ile ni ya miaka miwili iliyopita, maana Hesabu za Ukaguzi ni za miaka miwili iliyopita. Basi mnakaa hapa mnalalamika tu, Wizara hii sugu kwa kutokuzingatia. Lakini ni habari ya miaka miwili iliyopita, pengine wakati Taarifa inatoka yale yote yamesharekebishwa na kujibiwa. Mimi nadhani ule uharaka wa kuchukua hatua utatusaidia kidogo kurejesha imani.

Lakini hali kadhalika wasiorejesha masurufu ya safari nao washughulikiwe, mtu mpaka anabeba mpaka mamilioni lakini bado anapewa nyingine anasafiri. Nadhani haya ni ya taratibu za kawaida za nidhamu ya utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utawala bora ni pamoja na Serikali kufanya vizuri kazi zake nyingine muhimu ya kutengeneza mazingira mazuri ya uchumi kukua. Hili ni jukumu la msingi wa Serikali maana nimesema Serikali ina jukumu la Utawala lina jukumu la maendeleo. Tutahakikisha kwamba Serikali ya Awamu ya Nne inatekeleza ipasavyo jukumu lake hilo, na nakusudia baadhi ya mambo ya kufanya:-

1. Kuweka sera na mazingira bora ya kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi; uchumi haukui bila wawekezaji;

Ajira haitapatikana kama wawekezaji hawatafuatiliwa. Kwa hiyo, ndiyo maana tulisema wakati ule tutaunda Serikali ambayo itakuwa rafiki na wafanyabiashara si urafiki wa kunufaika Kikwete binafsi, ni urafiki kwamba watakuja wawekezaji wa ndani na wa nje ili wasaidie uchumi kukua, kazi ziweze kupatikana.

2. Kuweka sera nzuri zinazowezesha ukuaji wa uchumi wa kisasa;

3. Kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa mazingira ili kulinda uhai wa binadamu na viumbe, hili muhimu sana na mazingira kwangu mimi naona ni jambo la *priority* sana; *(Makofi)*

4. Kuweka mifumo bora ya kusuluhisha migogoro ya kibiashara;

5. Kuweka utawala mzuri wa sheria na wa haki;

6. Kuwa na taasisi za kudhibiti na kusimamia viwango na huduma na bidhaa;

7. Kuwa na sera nzuri za kifedha ili kuhamasisha uwekezaji na uzalishaji; na

8. Kutekeleza kwa dhadi sera ya uwezeshaji wa Watanzania wanyonge. Maana tusipokuwa nayo wako watu watakuwa watazamaji kama vile waliokuwa *National Stadium* kuangalia mpira wenzao wananufaika, wao kazi yao ni kupiga makofi tu au kulaumu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kazi ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne ni kukuza uchumi kwa lengo la kuongeza kipato cha Watanzania ili waishi maisha bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ninayoiongoza itatoa kipaumbele katika kujenga uchumi endelevu, wa kisasa, unaokua. Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya kazi kubwa katika eneo hilo na kutuachia msingi imara ambao sisi tutajenga juu yake. Hatutabomoa msingi huo bali Serikali yetu itatumia mafanikio hayo kama nyenzo ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi ndiyo mhimili wa uchumi wa nchi yetu hivi sasa. Zamani ilikuwa sekta ya dola, nadhani Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru hakasiriki kwa mabadiliko haya. Serikali ya Awamu ya Tatu imeweka mazingira mazuri ya ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi wa Taifa. Serikali ya Awamu ya Tatu imeweka mahusiano mazuri kati ya sekta binafsi na Serikali na inachukua hatua za kuboresha uwekezaji na biashara nchini. Aidha, Serikali ya Awamu ya Tatu imejenga mahusiano mazuri na sekta binafsi ambayo sasa imepewa fursa ya kushirikiana na Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini. Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza kazi hiyo nzuri. Tutajitahidi kuwa karibu na sekta binafsi kwa maslahi ya nchi yetu na kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu ndiyo uti wa mgongo. Kilimo ndiyo sekta mama. Sekta inayoajiri watu wengi na ndiyo inayoajiri watu wengi na ndiyo inayotuhakikishia upatikanaji wa chakula, bidhaa za kuuza nje na malighafi za viwanda. Sekta ya kilimo ndiyo inayotoa ajira kwa wananchi walio wengi. Serikali ya Awamu ya Nne itayaendeleza mazuri yote yaliyofanywa kuwa ni sekta ya kilimo. Vile vile, uhai na maendeleo ya sehemu kubwa ya wananchi yanategemea kilimo. Serikali sasa inatoa ruzuku kwenye mbolea na vile vile inatoa nafuu ya kodi kwenye pembejeo za kilimo na mifugo. Hili jema tutaliendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha mpango kabambe wa umwagiliaji maji. Tutauongezea fedha na wataalam ili tuufanikishe zaidi. Wakati huo huo pia umwagiliaji

wa asili ambao ni maarufu katika baadhi ya maeneo nao tutaufufua miundumbinu yake tutaisaidia ili iweze kuboresha kilimo. Huduma za ugani na masuala yanayohusu masoko nayo pia yatapewa kipaumbele na msukumo maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutachukua hataua za dhati kuboresha ufugaji wetu. Hatuna budi tutoke kwenye uchungaji wa kuhama hama na kugeuza nchi nzima malisho na sasa tuwe wafugaji wa kisasa. Siku ile nilipokwenda Kilolo kwa Profesa kule wa kampeini, nilikutana na Wamasai wa kwangu Chalinze kule, *yero roba eba,* maana tunafahamiana, Mbunge unafanya nini huku? Nikamwambia niko kwenye kampeni na wewe unafanya nini? Anasema mimi nimeleta ng'ombe huku. *(Makofi/Kicheko)*

Kule milima ya Udzungwa kule juu kule, wanatafuta malisho. Ng'ombe hanenepi, mfugaji hanenepi. Lazima kwa kweli tutoke hapo. Karne ya 21 hatuwezi kuendelea na ufugaji wa kuchunga. Tutachukua hatua za kuboresha malisho, upatikanaji wa maji, maana ndivyo vinavyowasumbua, tuboreshe huduma za dawa, majosho na minada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina mifugo mingi sana milioni 17, tukiboresha ufugaji itatoa mchango mkubwa sana katika Pato la Taifa. Lakini sasa hivi hakuna mchango wake ni mdogo sana. Serikali pia itawawezesha wavuvi waweze kupata zana bora na vifaa muhimu vya uvuvi wa kisasa ili waweze kutumia kwa ukamilifu rasilimali iliyoko Baharini kwenye Maziwa na Mito ambayo hatujaitumia vya kutosha.

Katika maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote wa Taifa siku zote kinachofanyika ni kuongeza mchango wa viwanda katika Pato la Taifa. Ukikiona uchumi unabaki kuwa na mchango wake mkubwa ni wa kilimo uchumi huo haukui sawa sawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuendeleza viwanda nao ni jambo la *agenda* muhimu. Hatuna budi kufanya hivyo, kwa viwanda vikubwa, viwanda vidogo, viwanda vya kati au sekta kuu za uchumi, lakini vitatusaidia kukuza ajira. Vitasaidia pia sekta nyingine kukua, kilimo watasindika mazao, tutaongeza thamani ya mazao yetu, mazao yanayoharibika yanaweza yasiharibike. Machungwa Muheza kule yanaharibika, tukiwa na viwanda vya *juice* na matunda tutakuwa tumeyanusuru. Kwa hiyo, ni mambo ambayo tutayawekea mkazo maalum. Serikali ya Awamu ya Nne itatengeneza mkakati kabambe wa kutekeleza sera ya viwanda nchini. Tunayo sera hivi sasa tunataka tujipange vizuri tuitekeleze kwa nguvu zaidi.

Tutachukua hatua za makusudi za kukuza sekta hiyo na Serikali itaendeleza na kuimarisha utoaji wa mikopo kwa viwanda vidogo na vya kati. Mipango ya mikopo na dhamana kwa sekta hiyo upo hivi sasa unasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania tutaufuatilia kwa karibu ili uweze kutekelezwa kwa kasi zaidi.Shirika la Viwanda Vidogo nalo makusudio yetu tuliwezeshe, tulisaidie ili liweze kutimiza ipasavyo matumaini ya watu.

Tukizungumzia uchumi wa kisasa hauwezekani bila ya sayansi na teknolojia. Serikali ya Awamu ya Nne itahimiza matumizi ya sayansi na teknolojia na kuwekeza

katika utafiti. Aidha, Serikali itashirikiana na sekta binafsi kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana kwa ajili ya taasisi na asasi mbalimbali zinazoshughulikia utafiti, Mfuko wa Sayansi na Teknolojia utaimarishwa kwa kuongeza mchango wa Serikali pia kuhamasisha wadau wengine nao kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila kitu kina manufaa yake, mageuzi ya kiuchumi nayo yamezua katatizo kidogo. Yameongeza tofauti ya mapato miongoni mwa wananchi. Sasa ninapowakuta wale wenyewe walioiva kwenye itikadi *the class in class struggles* hii inakuwa ni jambo kubwa. Lakini si jambo la kupuuzia tofauti hizi zitakapokuwa *civil struggle* zinaweza kuwa chanzo cha mgogoro na mitafaruku katika jamii. Hatuna budi tuchukue hatua. Jawabu si kuwanyang'anya walio nacho na kuwagawia wasionacho. Jawabu hilo itakuwa tunagawana umaskini wote na hakuna aliyepata. Maana unamnyang'anya yule ili wote tugawane na kwa sababu maskini ni wengi kuliko matajiri wote tutaishia kule. Changamoto yetu kubwa ni jinsi gani tutawasaidia wale wenzetu walio chini ili na wao waweze kulipa. Hiyo imekuwa ndiyo moja ya ahadi yetu kubwa ya kuwasaidia wanyonge katika jamii waweze kuinuka. Ahadi ile tunajiandaa vya kutosha kuitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kurekebisha na kutengemaza uchumi ni hatua ya mwanzo katika safari ndefu ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Serikali ya Awamu ya Nne itaendelea na hatua inayofuata ya kuongeza ushiriki wa Watanzania walio wengi katika uchumi wa Taifa lao.

Awamu ya Kwanza iliwashirikisha kwa mali ya umma unataifisha yote inakuwa mali ya umma, mashirika ya umma ndiyo Watanzania walivyoshiriki. Baada ya mageuzi ya uchumi tumeingia kwenye sekta binafsi. Lakini tusipokuwa waangalifu na hasa kwenye ubinafsishaji unaweza ukakuta Watanzania walio wengi wako nje ni watazamaji. Sasa tunachukua hatua za makusudi za kuwawezesha Watanzania. *(Makofi)*

Tutaitekeleza sera ya uwezeshaji iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu. Kadhalika tutawasaidia wawekezaji wadogo wadogo kwa kuchukua hatua kadhaa zifuatazo:-

1. Kuandaa utaratibu mzuri zaidi wa kutoa leseni za biashara, maana naambiwa siku hizi hata wageni wamekuwa wamachinga nchini. Hilo ni suala la utoaji wa leseni tu; *(Makofi)*

2. Pia tutarekebisha mifumo ya udhibiti ili udhibiti usizuie sekta binafsi kukua;

3. Tutaandaa mazingira mazuri ya kufikisha taarifa muhimu za masoko;

4. Tutaitaka mikoa ianzishe vituo vya kufanikisha biashara na uwekezaji mikoani, nimeona Mkoa wa Kilimanjaro umefanya vizuri na mikoa mingine nayo imewahi kufanyia hivyo; *(Makofi)*

5. Kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali ikiwemo kutoa misaada na upendeleo maalum wa mikopo midogo midogo na hasa ya kati kwa vijana, wanawake na Watanzania wengine wanaohangaika kujikwamua kimaisha na kujitoa kwenye umaskini; *(Makofi)*

6. Tutaendelea kuboresha miundombinu inayogusa shughuli za biashara ndogo ndogo na za kati;

7. Kadhalika tutahamasisha na kuhimiza kutoa motisha kwa shughuli za usindakaji nchini ili kuongeza thamani ya mauzo nje. Ni aibu ndugu zangu kuendelea kuuza korosho ghafi. Unamuuzia mtu anakwenda kuchukua wanawake tu anawapa mashine ndogo ndogo wanabangua halafu anauza yeye. Hivi hata hili hatuliwezi? Lakini nalo lina matatizo kweli kuna watu ambao wanaishi kwa kuuza kule kila mkifanya jitihada hizo wanahujumu. Ndiyo mapambano yenyewe; *(Makofi)*

8. Kuhamasisha, kuhimiza na kutoa motisha kwa mafunzo ya kiufundi yanayolenga kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji ikiwemo uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi;

Mheshimiwa Spika, tutawezesha Watanzania kwa makundi. Kundi la kwanza ni la Watanzania wasomi, walio ndani na nje ya nchi yetu. Zamani ilikuwa mtu akitoka Chuo Kikuu, kazi ya Serikali inakungoja. Leo hali si hiyo. Serikali inaweza kukusomesha, lakini haikupi ahadi ya kazi. Wengi inabidi watafute kazi kwenye sekta binafasi au wajiajiri wenyewe. Na wapo ambao wanahangaika na kusaga lami japo wamesoma vizuri na kuwa na ujuzi wenye soko. Kwa mfano, utamkuta mtu anayo shahada ya kilimo, ufugaji au uvuvi lakini yuko mjini anatafuta kazi ya kuajiriwa na kukaa ofisini kwenye kiyoyozi. Napenda leo nitoe changamoto na ahadi kwa wasomi wetu hao, wenye fani mbalimbali kama vile kilimo, mifugo, uvuvi, uhandisi, ubunifu wa majengo, sheria, uhasibu na kadhalika. Katika dunia ya utandawazi na ushindani unaoambatana nao, Watanzania wasomi watabaki nje iwapo hawatakuwa wabunifu zaidi, wakaungana na kuanzisha kampeni kubwa za wazalendo. Bila hivyo hawataweza kuhimili ushindani wa makampuni yaliyokwisha kuimarika au yanayotoka nje ya nchi. Lakini wakikubali kuungana na kuanzisha kampuni kubwa zinazoendeshwa kwa misingi halisi ya kibiashara na sio ubabaishaji, Serikali kupitia vyama vya taaluma zao, itawaunga mkono, itawasaidia na itawawezesha. Serikali ya Awamu ya Nne itakaribisha mawazo kutoka kwa vyama vya kitaaluma juu ya namna bora ya Serikali kufikia lengo hilo. Ninataka wasomi wetu waweze kuhimili ushindani na wawe kiini cha wajasiriamali wasomi na wakubwa nchini.

Kundi la pili la Watanzania tutawasaidia na kuwawezesha ni la wenye miradi midogo midogo sana, miradi midogo na miradi ya ukubwa wa kati. Mazuri mengi yamefanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu kama vile sera ya uwezeshaji wananchi, sera ya uwekezaji mdogo na wa kati na mfuko wa udhamini kwa mikopo ya mitaji midogo na ya kati. Yote haya na mengine mengi, tutayaendeleza kwa jitihada kubwa.

Lakini wote ninaowasaidia msemo tunasema hivi, ukibebwa shikilia. Maana inawezekana kabisa ukawasaidia watu, baada ya muda fedha huzioni na mradi hakuna. Sasa huyu ndiyo yule anayebebwa, anayejilegeza hatutakuwa na msaada wala huruma na watu wa aina hii, ni jitihada tutafanya.

Katika ilani ya Chama cha Mapinduzi tumelizungumzia sana suala la ajira, tutaendelea na jitihada za kuongeza ajira Serikalini na katika sekta binafsi na kama nilivyoeleza tutatengeneza mazingira mazuri kwa sekta binafsi kukua, uwekezaji kuongezeka ili ajira iweze kupatikana.

Ndugu zangu ushirika ni nguzo muhimu ya kuwawezesha wanyonge kuwa na sauti na hivyo kuweza kupambana na umaskini na Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya kazi kubwa na nzuri kuunda upya Ushirika nchini na kuhuisha Sera na Sheria ili kuweka mazingira yatakayochochea kujengeka kwa vyama huru vya Ushirika vinavyomilikiwa na kuendeshwa na wanaushirika wenyewe. Serikali ninayoiongoza itaendeleza jitihada hizi pamoja na kuendelea kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi kujiunga na vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, huduma za jamii, elimu, kuendeleza huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji na kadhalika itaendelea kuwa ni jambo la kipaumbele cha juu. Elimu tunaendeleza, tutaendeleza kazi nzuri iliyofanywa kwenye elimu ya msingi, elimu ya sekondari, tutaongeza vijana kwenye shule, tutaboresha taaluma na kuongeza viwango vya kufaulu maana tusifanye ile hadithi ya wingi si hoja mnaweza mkawa na shule nyingi lakini kiwango cha elimu kikawa chini, tutapanua lakini pia tuta-*focus on* kuboresha kiwango cha elimu.

Tutaongeza ajira ya ualimu katika shule za msingi na shule za sekondari, sekondari za wananchi zina tatizo kubwa sana la walimu, tutaongeza kasi ya kupata walimu. Siku moja nilikuwa nasoma kwenye gazeti moja hivi wanashutumu hatua za Serikali za jitihada za haraka kuwa na walimu wengi, wanasema huko ni kudhoofisha elimu, lakini sasa shule zipo tayari, tuanze hatua za haraka ili watoto walioko darasani wapate elimu, tutaendelea kuwaimarisha walimu waliopo. Tutashirikiana na wazazi na wadau wengine wa elimu kujenga nyumba, vyumba vya madarasa na hasa hasa kutatua tatizo la nyumba za walimu. *(Makofi)*

Tumejenga shule nzuri, lakini ile shule nzuri, ile nyumba anayolala mwalimu inatisha, sasa uzuri ule wote unakuja kuharibikia pale, sasa tunataka tuyaweke mambo sawa, tutaongeza ruzuku inayotolewa hivi sasa kwa ajili ya kugharamia gharama za kuendesha shule, tutaimarisha Taasisi ya udhibiti wa ubora wa elimu, inayotolewa, ziko shule nyingi siku hizi na zina majina makubwa makubwa nyingine *International Academy* sasa hatuna hakika ya ubora wa elimu kwenye ile, nataka mamlaka hizi zichangamke tuthibitishe ili watoto wetu wapate elimu ya kweli ili wasiwe tu kwamba wameshiriki, nitatoa fursa na motisha kwa sekta binafsi, taasisi za dini, watu binafsi na mashirika binafsi yanayowekeza kwenye elimu wanatoa mchango mkubwa, tuwawezeshe ili waweze kutoa mchango zaidi. *(Makofi)*

Tutaimarisha bodi ya mikopo ya elimu ya juu, inalalamikiwa nadhani hatuna budi tuchukue jawabu, tutafute hatua za kutatua matatizo yaliyopo pale ili tusiwe na watu wanaonung'unika kila siku tu, kwa majawabu yanayoweza yakafanyika. Tujenge angalau chuo kikuu kingine, mwaka huu fundisho kubwa, vijana wetu wengi wameshindwa kupata nafasi kwa sababu ya nafasi finyu, tutakuza mafunzo ya ufundi stadi yatusaidie kutengeneza ajira katika mzunguko wangu maji limekuwa ndio tatizo kubwa., tutalikabili kwa nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Tumetoa ahadi asilimia 90 mijini, asilimia 65 vijijini tutatekeleza ahadi yetu hii, tutaendelea kuboresha huduma ya afya nchini, tutaongeza zahanati, tutaongeza vituo vya afya, tutaongeza hospitali, tutaboresha upatikanaji wa dawa, kadhalika tutapambana na tatizo la UKIMWI kuongeza uhamasishaji, kuongeza elimu, lakini kutoa dawa kwa wale walioathirika, tutaendelea kujenga uwezo wetu siku hadi siku. Tutaendelea katika awamu ijayo kuyaangalia maslahi ya watoto yatima tuhakikishe wanasoma, tuhakikishe wanapata matibabu. Tutaendelea kuhakikisha kwamba walemavu nao wanapata haki, kuhakikisha kwamba hawabaguliwi wala hawanyanyapaliwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo kundi la wazee. Wazee ni hazina kubwa ya Taifa lolote. Wao ndio waliotujengea misingi ya Taifa tuliyo nayo hivi sasa. Zipo hatua zilizochukuliwa za kuwawezesha kupata huduma za afya bila malipo na kwa wale wa Mijini kutotozwa kodi ya pango kwa zile nyumba wanamoishi wenyewe. Jamii yoyote iliyostaarabika inalo jukumu la kuwaenzi na kuwatunza wazee. *(Makofi)*

Jukumu la kwanza linaanza katika familia na wanajamii wa karibu wa mzee anayehusika. Tunawaomba wasikwepe jukumu hilo asilia na la mila za kiafrika na kuwaacha wazee wao wanahangaika barabarani. Lakini Serikali nayo itatimiza wajibu wake na tunakusudia kutengeneza utaratibu wa kutekeleza sera ya wazee ambayo tayari ipo Serikalini. Serikali itahakikisha kuwa kunakuwepo utaratibu na mipango itakayowawezesha wazee kupata huduma muhimu kwa wepesi zaidi na kwa gharama nafuu, kwa kuzingatia taratibu, mila na utamaduni wa jamii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la jinsia, Serikali inatambua bayana na inaahidi kuzingatia nafasi ya wanawake katika maendeleo. Tutaongeza, awamu kwa awamu, ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi nyingine za maamuzi, niliahidi wakati wa kampeni kwamba Baraza la Mawaziri litakuwa na sura za wanawake wa kutosha, kazi hiyo sijaianza ndio tumepata Waziri Mkuu tu, lakini nitahakikisha ahadi yangu naitimiza ili msije mkanisuta. *(Makofi)*

Tutaendelea kuwahamasisha wanawake wazitumie fursa za kisiasa katika nyaja mbalimbali zikiwemo za uchaguzi katika ngazi zote bila kusahau kuongeza nafasi na fursa katika ngazi za uteuzi kwenye utawala, uongozi na menejimenti ndani ya Serikali na taasisi zake.

Kadhalika, tutatekeleza ahadi ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Tutatengeneza na kutekeleza mikakati kabambe kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wajikwamue na umaskini na uduni wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utalii. Utalii ni moja ya sekta ambazo ni mhimili wa uchumi wa nchi yetu hivi sasa. Serikali yangu inakusudia kuendeleza sekta hii ili iongeze mchango wake kwenye Pato na maendelezo ya Taifa letu, tunakusudia tuboreshe huduma kwa watalii, malazi, vyakula, usafiri na bidhaa mbalimbali hizi za zawadi tutafanya lakini liko jambo kwenye mahoteli ambalo sijafurahishwa nalo sana, nimeona mameneja wengi wageni tu, sitaki kuonekana kama vile sipendi wageni lakini basi hata Meneja msaidizi jamani, hata Meneja wa nini mdogo mdogo hivi bado wageni tupu na wengine ndio wanafika mahali hata maji wanaagiza kutoka kwao. *(Makofi)*

Sasa nasema katika sekta hii Waziri atakayeteuliwa kuiongoza Wizara ya Utalii nitamwomba uwezeshaji wa wazawa katika kuendesha hoteli na sekta hii uzingatiwe. Haitoshi kujigamba peke yake kuwa Tanzania ina mbuga kubwa na nzuri za wanyamapori, milima, mabonde na fukwe zenye mchanga mweupe. Ni kweli tunapaswa kuulinda na kuuendeleza urithi huu lakini zaidi ya hayo tunapaswa kutumia urithi huu kwa manufaa ya nchi yetu.

Tunapaswa kuboresha huduma kwa watalii kama vile malazi, chakula, usafiri na bidhaa za kumbukumbu za kuwauzia watalii. Tunapaswa kukaribisha wawekezaji wa ndani na nje watakaojenga hoteli zenye hadhi ya Kimataifa kuanzia nyota nne hadi tano. Tunahitaji kujenga miundombinu ya kuwafikisha watalii katika maeneo ya kitalii kwa urahisi. Tunapaswa kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya utalii ili tuongeze idadi ya watalii na mapato kutoka utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya mazingira, Serikali ya Awamu ya Nne itatoa msukumo maalumu kwa hifadhi ya mazingira kwani athari zake pale tulipopuuzia zinaonekana wazi. Mvua haba, rasimali maji inazidi kupungua na ukame unaongezeka. Ndugu zangu kila mmoja wenu ajaribu kukumbuka ule mto ambao zamani alikuwa anaoga unatiririka maji toka Januari mpaka Desemba, mingapi bado ipo hivyo, rasilimali ya maji imepungua na tusipochukua hatua za hifadhi ya mazingira miaka kumi ijayo tutakuwa na mgogoro mkubwa wa maji, si kwa sababu hatukutandaza mabomba, ila mabomba yale yanafoka hewa maji hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio maana suala la mazingira inabidi tulipe mkazo na msisitizo maalum, tutaiongezea Wizara inayohusika na mazingira, uwezo na mamlaka ya usimamizi. Tutaendeleza kampeni ya upandaji miti, tupande miti Watanzaia kama vile wendawazimu, manufaa yake tutayaona, kuna wakati mmoja mzee Malecela alipokuwa Mkuu Mkoa wa Iringa alipata sifa kubwa kwa kupanda miti kwa wingi, mifano hiyo ipo ni kitu kinachowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendeleza kampeni ya upandaji miti na kuhimiza tabia ya kutokata miti ovyo au kuchoma misitu ovyo. Lakini ili kupunguza mahitaji ya kuni na mkaa, tufanye jitihada ya kuendeleza matumizi ya nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka arobaini iliyopita, Tanzania Bara ilikuwa bado na misitu mingi, chemchem na vijito vingi. Sehemu kubwa ya ardhi yake ilikuwa

imefunikwa na maji na majani. Leo hali ni tofauti kabisa na kwenye baadhi ya maeneo hali inatisha.

Mheshimiwa Spika, uchomaji misitu na ukataji ovyo wa miti vimesababisha vyanzo vya maji kukauka, mito kupungua maji na baadhi ya viumbe kuathirika na hata kutoweka. Hatuwezi kuendelea kuwa watazamaji au washangaaji wa vitendo hivi vya hujuma dhidi ya misitu na uhai wa Taifa letu na wala uhuru wa Mtanzania kuishi popote katika nchi yake haujumuishi pia uhuru wa kuharibu mazingira sehemu fulani ya miti na kuhamia sehemu nyingine. Hakuna uhuru wa kuharibu mazingira kwa namna yeyote ile. Serikali ya Awamu ya Nne inaagiza yafuatayo:-

1. Kila kijiji kipande miti katika vyanzo vya maji;

2. Wizara ya Ujenzi ihakikishe miti inapandwa pembeni mwa barabara na katika maeneo karibu na madaraja;

3. Wizara yenye dhamana ya maliasili iweke utaratibu mzuri, unaofuatiliwa na unaopimika na upandaji miti na majani;

4. Wizara yenye dhamana ya ardhi ihakikishe machimbo ya mchanga na kokoto hayako katika maeneo karibu na vyanzo vya maji au katika mabonde na kingo za mito;

5. Wizara ya Madini ihakikishe inasimamia vizuri na kuyatolea taarifa za kila mwaka maeneo yote yenye machimbo ya madini ili kufuatilia na kujihakikishia kuwa wachimba madini, wanazingatia matakwa ya leseni zao za uchimbaji madini na hasa masharti ya hifadhi ya mazingira;

6. Wananchi wanaoishi katika maeneo yenye viwango vizuri vya mvua za kutosha waongeze bidii na kasi ya kupanda miti;

7. Wizara yenye dhamana ya mazingira iandae ripoti za kila mwaka kuhusu hali ya mazingira nchini ikijumuisha mafanikio na changamoto;

8. Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji zitekeleze kwa vitendo agizo la siku nyingi la kupanda miti ya vivuli na matunda; na

9. Watu binafsi, mmoja mmoja au katika makundi, waanzishe kampeni ya kupanda miti kama zao la biashara.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo lazima hatua zichukuliwe maalum kulinda na kuhifadhi mazingira, nilipokuwa Iringa wakati wa kampeni, nilisema kwamba asilimia 80 mpaka 90 ya uwezo wa kuzalisha umeme wa maji unategemea mito inayoanzia kwenye *Livingstone Mountains.*

Leo hii Kihansi nilikuwa natapata taarifa juzi ina uwezo wa kutoa *megawatt 180,* sasa inatoa 57, Mtera ya *megawatt 80* inatoa 37, Kidatu ya *megawatt 200* iko chini 100

maji hayatoshi. Nasema kwamba tuchukue hatua maalum kwenye maeneo haya, Mto Ruaha ambao ulikuwa ni mto unaotiririka maji mwaka mzima wakati mmoja tulikuwa na programu moja kwenye *television* yao, nyani wanacheza mle kwenye mchanga, viboko wanakufa hatuwezi kuendelea hivyo. Kwani hali imeanza kuwa mbaya sana hata kuanza kuhatarisha ustawi na maendeleo ya sekta nyingine.

Eneo mojawapo ni Bonde la Mto Ruaha ambalo linahusisha vyanzo vya mito yote mikubwa nchini. Tumeshuhudia hali ya Bwawa la Mtera inavyoendelea kuwa mbaya. Aidha, Mto Ruaha mkuu umeanza kukauka katika baadhi ya maeneo. Itabidi uongozi wa Serikali katika ngazi zote uwajibike zaidi kuhakikisha kuwa uharibifu wa mazingira unaosababisha hali hii ya kutisha unakomeshwa.

Eneo lingine ni lile linalozunguka Ziwa Victoria. Hivi sasa tunatekeleza mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mkoa wa Shinyanga. Taarifa za kitaalamu zinaonyesha kuwa pamoja na umuhimu wa Ziwa hilo, uchafuzi wake unaongezeka, hata leo nilikuwa nasikiliza kwenye *television* au kwenye redio kipindi kinachoelezea uchafuzi wa mazingira kwenye Ziwa hilo. Ndugu zangu hatuna budi tulishughulikie kwa dhati tatizo la mazingira, hifadhi ya mazingira kwa sababu ndio uhai wetu, vinginevyo hatuna *future.* Serikali itahakikisha kuwa uongozi wa Mikoa yote inayozunguka Ziwa hilo unashirikiana na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa na wananchi kuhifadhi Ziwa hilo linalotumiwa na idadi kubwa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, uchumi unaopaa, baada ya mafanikio ya Awamu ya Tatu, haitarajiwi kuwa Serikali ya Awamu ya Nne kwamba italegeza kamba na kuupuza misingi iliyotuletea mafanikio tunayojivunia. Najua maneno mengi yamesemwa na watu wanaodai kwamba wananifahamu vizuri Jakaya Mrisho Kikwete na jinsi gani nitakavyolegeza mambo.

Napenda kuwahakikishieni kuwa watu hao wamepotea sana. *I may be wearing a smile but it could be very deceptive, firm on issues.* Nina msimamo kwenye masuala ya msingi. Kwa sababu sina namna ya kufanya uso wangu uwe umekasirika, nitakuwa na *smile* lakini bado nitakuwa na msimamo. Maana kila kitu ni maumbile ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Wakati wa kampeni wapo baadhi ya wapinzani waliothubutu kwa kukosa shukrani, kusema eti Serikali ya Awamu ya Tatu ilikuwa inatekeleza sera zinazobuniwa Washington. Serikali ya Awamu ya Nne, kwanza si kweli katika mahusiano yetu na Mashirika ya Kimataifa haya, moja ya sifa kubwa ya Tanzania na ndio maana *World Bank IMF* wanaitolea mfano Tanzania. Sisi tunamiliki mipango yetu. *(Makofi)*

Ni sisi wenyewe tunaosema tunataka nini wao wanatuambia hiki fedha tunazo, hiki fedha hatuna na Serikali ya Awamu ya Nne haitaogopa kubuni na kutekeleza sera na mikakati ya maslahi kwa ukuaji wa uchumi na maisha bora kwa kila Mtanzania eti kwa vile zinaungwa mkono au kufadhiliwa na nchi tajiri na Mashirika ya fedha ya Kimataifa. Uwezo wetu una kikomo. Pale tulipoishiwa ndipo tunaomba msaada. Hili hatutaliacha! *(Makofi)*

Lakini hatutafanya lolote lisilo na maslahi kwa Taifa letu kwa kuwaogopa au kutaka kujipendekeza kwa wakubwa hao. Lakini vilevile hatutaacha kufanya lolote la maslahi kwa Taifa na Watanzania kwa vile tu linakwenda sambamba na ushauri wa Mashirika ya fedha ya Kimataifa. Hatutafanya maamuzi kwa kutaka kupendwa; lakini tutafanya kila maamuzi kwa kigezo cha msingi cha maendeleo na maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali ya kusukumwa na hoja ya kukuza uchumi haraka ili kupiga vita umaskini, tunasukumwa pia na ukweli wa nguvu za utandawazi na ushindani mkubwa katika masoko ya Kanda na ya Kimataifa. Hivyo basi, sote tuunganishe nguvu zetu ili tuongeze uzalishaji, tuongeze uwekezaji, tuongeze mauzo nje, tuongeze ubora wa mazao na huduma zetu na tuongeze kasi ya ukuaji wa uchumi wetu ili upae. Hakuna kurudi nyuma. Kasi mpya inayozungumziwa ni ya kusonga mbele na siyo kuserereka na kurudi nyuma kwa kasi.

Ndugu zangu, kuhusu michezo nataka niseme yafuatayo:- Kwanza, michezo ni furaha, michezo ni afya, Watanzania wanapenda sana michezo, ila wamekuwa wanakosa furaha kwenye michezo na furaha tumekuwa tunaikosa kwa sababu ya timu zetu kutofanya vizuri. Lazima tutoke huko, na inawezekana. Tuwe makini kuendeleza michezo. Tutahimiza maendeleo ya michezo Shuleni na pale inapowezekana katika sehemu za kazi. Shule ziwe mahali pa kubaini vipaji vya sanaa na michezo na kuwaendeleza. *(Makofi)*

Tutafanya jitihada kwa mazungumzo kama nilivyozungumza katika Mjadala mpana ili tuondoe migogoro na matatizo yanayokabili Vyama vya Michezo na vilabu vya michezo. Hatuna uwezo mkubwa, lakini tutafanya jitihada ya kuviwezesha Vyama vya Michezo ili Tanzania iweze kushiriki vizuri na isiwe ni msindikizaji katika mashindano mbalimbali ya michezo ya ulimwengu. Pamoja na hayo nitaanzisha Mjadala wa kitaifa na kuendeleza michezo nchini. Wadau wote washiriki na Watanzania, tukubaliane juu ya mustakabali wa michezo nchini mwetu. *(Makofi)*

Nikisema hayo sina maana kwamba sasa wenye vilabu vya michezo wawe wanakula hela zote za vilabu vyao wakingojea Serikali itafanya hiyo kazi, hapana. Tutakubaliana maeneo gani tutatolea michango na ahadi naitoa mimi, ni kwamba tutatoa michango katika kuendeleza taaluma. *(Makofi)*

Kama Chama cha Mpira wa Miguu kina matatizo ya fedha za kumlipa Kocha, hili mimi nitasaidia. Lakini sio na kuisafirisha timu sasa warudi kwangu, hapana. Fedha wanazokusanya *National Stadium* wazitumie kufanya kazi hiyo. Kama ili kuendeleza michezo katika mashule unahitaji walimu wa michezo tutawekeza katika kufundisha walimu wa michezo. Lakini kuwapeleka kwenye UMITASHUMTA haiwezi kuwa kazi ya Serikali. Tutapata fursa ya kukaa pamoja na wadau mbalimbali ili tuyazungumze masuala haya ili tukubaliane namna ya kuendeleza michezo nchini na muafaka tutakaokubaliana. Basi wote kwa pamoja tukubaliane kwamba hivyo ndivyo

tutakavyokuwa kwa sababu, timu zinaposhindwa wasidhani tu wale viongozi wabovu kwenye vile Vyama au Vilabu, wanawakasirisha Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Tutaendeleza Sekta ya Utamaduni na burudani kwa ujumla. Miongoni mwa mambo ambayo tutayaangalia kwa karibu ni haki na maslahi ya wasanii ili kazi kubwa waifanyayo iwe na tija kwao.

Mheshimiwa Spika, lugha yetu ya Kiswahili imeanza kupata umaarufu Afrika na dunia na baada ya kukubaliwa kwamba ni lugha rasmi maombi kwenye Ubalozi wetu pale Addis Abba wa Wafanyakazi wa *African Union* kutaka kufundishwa Kiswahili ni makubwa sana. Lakini nchi kadhaa duniani zimeomba Walimu. Libya imeomba Walimu 1000, Kongo imefanya hivyo hivyo, zipo nchi kadhaa zinaomba tuwapelekee Walimu. Nadhani maombi tuliyonayo yanakaribia 3,000 hivi. Ajira hiyo! *(Makofi)*

Serikali itajihaiddi kuongeza mchango katika kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini, lakini pia kuwezesha lugha ya Kiswahili kuweza kutumika Afrika na Duniani. Tunayo mawazo hatujayakamilisha, nilikuwanayo wakati tulipokuwa *Foreign Affairs* kwamba pengine mahali kama Addis Abba hivi tungeanzisha *Tanzania Cultural Centre,* ambayo kazi kubwa pale ni kufundisha Kiswahili na sisi bado tunaweza tukafanya, lakini mawazo bado hatujayakamilisha.

Umoja wa Afrika umekubali Kiswahili kuwa moja ya lugha zake kuu. Aidha, nchi za Kanda ya Maziwa Makuu zimekubali kutumia na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kuwa juhudi hizi zinaendelezwa na kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inakua nje ya mipaka ya Afrika. *(Maakofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendeleza Miji ni jambo tutakalolipa uzito unaostahili ili tuwe na Miji mizuri, Miji safi na Miji iliyo salama. Sote tumeona jinsi ambavyo dhana ya mipango Miji inavyopuuzwa na kukiukwa na baadhi ya wananchi hasa wenye uwezo. Manispaa na Halmashauri zetu *open space* zinagawiwa tu! Jambo hili naweza kuahidi wale Mabwana Ardhi wanaogawa, waache. Kwanza wanatukanisha *profession* yao, wanaidharaulisha sana! Wewe Bwana Ardhi ndio unatakiwa kuwa msimamizi wa kukataa *open space* isigawiwe, matokeo yake sisi tuna Miji ambayo huwezi kutengeneza *park,* sehemu ya watu kupumzika, kila mahali tumegawa, hakuna mahali pa shughuli nyingine. Mifano ya ukiukwaji wa Kanuni bora za Mipango Miji ni kama ifuatavyo:-

1. Nyumba na kuta zinajengwa katika maeneo ya mikondo ya maji;

2. Makazi ya watu yanaanzishwa katika maeneo ya hifadhi ya barabara;

3. Maeneo ya wazi, ya bustani na michezo ya hifadhi ya barabara;

4. Mifugo inawekwa, na hata kuchungwa, Mijini karibu na makazi ya watu;

5. Majumba marefu yanaruhusiwa kujengwa katika maeneo ambapo huduma za majitaka hazitoshelezi;

6. Makazi yanaanzishwa pasipo kuweka mifumo mizuri ya barabara na huduma nyingine muhimu hasa za maji taka na usafi wa mazingira;

7. Maeneo kwa ajili ya huduma za maduka, masoko, hospitali, shule, na maeneo ya ibada na makaburi, ama yanatengewa maeneo finyu au husahauliwa kutengwa, ama yakitengwa bado yanamegwa kwa ajili ya matumizi mengine;

8. utupaji taka na mifuko ya plastiki hufanywa ovyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tusipokuwa waangalifu Miji itakuwa kama pori la majengo yasiyokuwa na mpangilio wala huduma zinazohitajika. Unakuta mtu amejenga jumba la gorofa nane mahali ambapo ule mfumo wa maji taka hauna uwezo wa kuhimili jengo la gorofa nane, lakini Bwana Ardhi amegawa. Kuna watu wengine wanajenga nyuma za gorofa kwenye maeneo ambayo nyumba zote ziko chini, akikaa juu anawachungulia wenzake. Kama tumeamua kwamba tunabadili maeneo haya, sasa yatakuwa ni nyumba za aina hii, mnabadili yote lakini msifanye hivi Kanuni hizi lazima sasa mabwana ardhi warudi kwenye *basics* kama walivyosomea. Lakini tutaangalia uwezekano wa kuanzisha upya chombo cha fedha kitakachotoa mikopo ya kujenga na kununua nyumba. Tulikuwanayo Benki ya Nyumba ikafa na ndio maana vishawishi vya rushwa vimekuwa vingi kwa sababu mtu anataka nyumba, basi ukipata *under the carpet* unapata nyumba, tunataka tuwaondoe watu kwenye mazingira hayo tuanzishe taratibu rasmi.

Serikali ya Awamu ya Nne itazitaka Halmashauri zote zishughulikie jambo hili haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, tutaendeleza huduma za kiuchumi kama barabara, nishati, simu na kadhalika, kazi kubwa imefanyika kuhusu barabara na tumeahidi sana kuhusu barabara kwenye *line* yetu. Yale tuliyoyaahidi kwenye ilani tutayatekeleza kwa sababu yametengenezwa kiutaalam tukiamini kwamba uwezo upo maana kuna wakati wamesema kwamba eh! huyo mgombea anaahidi huyu! Lakini yote niliyokuwa nayasema yako kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tutajitahidi kujenga uwezo kama ilivyokusudiwa ili ahadi zetu kwenye kuendeleza barabara yaweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye nishati, tutafanya jitihada ya kujaribu kutafuta majawabu ya matatizo ya umeme nchini, lakini pia tutafanya jitihada katika awamu ya nne kuharakisha kupata umeme kutokana na makaa ya mawe ya Mchuchuma. *(Makofi)*

Tunalisema hili kwa sababu ni vizuri tuwe wakweli kwamba sasa umeme wa maji matumaini yake ni ya mashaka na maadamu raslimali ya makaa tunayo, tuchangamke katika kutekeleza mradi huo, tufanye jitihada ya kuelekeza nguvu zetu huko. Kadhalika tutaendelea kufanya jitihada ya kutafuta vyanzo mbalimbali vya kukidhi mahitahi ya umeme. *(Makofi)*

Katika Awamu ya Nne, pia tutafanya jitihada ya kuyapatia Makao Makuu ya Wilaya ambazo bado umeme, kazi kubwa imefanyika wakati wa kampeni, tulikuwa na Wilaya kama 20 kwa sababu sasa ziko chini ya 13, naamini kwenye miaka 15 ijayo tunaweza kuzimalizia. Kadhalika tutaendeleza jitihada za kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Ruvuma kwenye Gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, kuhusu sera ya Mambo ya Nje, tunawaahidi Watanzania kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba nchi yetu ina marafiki wengi kadri inavyowezekana. Kuna urafiki na Mashirika ya Kimataifa kwa manufaa ya nchi yet. Tumeifanya kazi hiyo vizuri na tutaiendeleza kwa ubora zaidi. Tutasimamia kwa ukaribu zaidi utekelezaji wa ile sera ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni kwamba tutasimamia kwa karibu mchakato mzima wa mjadala wa kuanzishwa kwa shirikisho ili tuingie kwenye shirikisho tukiwa na uhakika kwamba tunanufaika. Sababu za kuingia kwetu kwenye shirikisho ni maslahi yetu, lakini tutafanya jitihada tuhakikishe kwamba katika kutafuta maslahi yetu hatucheleweshi mchakato mzima. *(Makofi)*

Kadhalika, tutaendeleza ushiriki na uhusiano wetu katika Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika; tutahakikisha pia kuwa Tanzania inaendelea kuishi kwa ukamilifu na kuwa mwanachama wa Umoja wa Afrika na inaendelea kushiriki kwa ukamilifu katika utatuzi wa migogoro Barani Afrika hususani katika michakato ya kuleta amani katika nchi za maziwa makuu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania itaendelea kushiriki kwa ukamilifu kwenye shughuli za Umoja wa Mataifa. Hivi sasa nchi yetu ni mwanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na kesho kutwa tarehe 01 tutachukua Kiti cha kuwa Rais wa Baraza la Usalama. Katika kipindi hicho Tanzania inatarajia kuwasilisha ajenda ya Usalama na Usuluhishi wa Migogoro katika eneo la Maziwa Makuu ili ijadiliwe na Baraza la Usalama na hatimaye tupate Azimio la Baraza la Usalama itakayoweka wajibu wa Umoja wa Mataifa katika kusaidia usalama na maendeleo ya eneo letu. *(Makofi)*

Kadhalika, tunaahidi tutaongeza ushiriki wa Jeshi letu katika Majeshi ya Kulinda Amani ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika. Hivi sasa tunashiriki, lakini ninachoahidi tutaendelea kushiriki kwa nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu wa nchi yetu ni moja ya agenda kubwa, maendeleo ya uchumi pia yanategemea sana kuwepo na utulivu nchini. Pamoja na matukio ya hapa na pale, nchi yetu kwa ujumla imetulia na ni wajibu wetu kuendeleza utulivu huo kwa kufanya yafuatayo: - Kwanza, kujenga mazingira mazuri ya kazi kwa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Pili, kuendeleza juhudi za kuwa na Majeshi ya Ulinzi na Usalama yaliyo imara na yenye nidhamu ya hali ya juu na utii, yenye utaalamu na yenye zana za kisasa za kufanyia kazi. *(Makofi)*

Tatu, tutaongeza uwezo wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya kupambana na majambazi na kuzagaa kwa silaha ndogondogo ambazo zimekuwa zinatumika sana katika uhalifu dhidi ya raia wema ndani ya nchi. Tatizo hili tutalivalia njuga, tutaangalia maslahi ya Wanajeshi wetu katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Nne, kuanzisha na kutoa vitambulisho vya uraia. Tano, tutaongeza kasi ya kurejesha wakimbizi makwao. Nataka nilifafanue hili, nikisema hivi, watu wasije wakasema; Rais sasa amesema asubuhi watu watarundikwa kwenye malori watapelekwa, hapana. Ziko taratibu zilizopo. Tunaiona kasi yake ni ndogo, tunataka kasi iongezeke ya watu kurudi kwao hasa maeneo ambayo tayari amani ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema mengi, nadhani kwa leo inatosha, naomba nimalizie kwa kuwahakikishieni tu kuwa nafahamu vizuri sasa ukubwa wa heshima na uzito wa majukumu niliyokabidhiwa na Watanzania wenzangu. Ninayafahamu matarajio ya Chama changu cha Mapinduzi na ninawaahidi kwamba nitaongoza kwa dhati utekelezaji wa ahadi zetu kwa wananchi kama tulivyozitaja kwenye Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayatambua matarajio ya Watanzania wenzangu walipoitikia wito wa "Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya." Nitajitahidi kwa uwezo wangu wote nisiwaangushe kwa matumaini hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayajua matarajio ya nchi jirani, Bara la Afrika na Dunia kwa Awamu ya Nne ya Uongozi wa Taifa letu, ninajua matarajio ya Wahisani wetu na Wawekezaji wa ndani na wa nje, najua wananisikiliza kwa makini wakitaka kujiridhisha iwapo nitavijaza viatu alivyoviacha Rais mstaafu Mheshimiwa Benjamini William Mkapa. Nitajitahidi ingawa viatu hivyo ni vikubwa kwangu, lakini viatu hata vikiwa vikubwa si unaweka na karatasi mbele? *(Kicheko/Makofi)*

Kwenu nyote na kwao wote, naahidi kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, maana ndiye mwezeshaji wa yote na kwa ushirikiano wa Bunge hili na kwa ushirikiano wa wananchi wa ujumla, naweza kutimiza matarajio ya kila mmoja wetu. *(Makofi)*

Tanzania yenye neema tele inawezekana, maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana, kila mmoja wetu atimize wajibu wake. *(Makofi)*

Mungu ibariki Afrika,
Mungu ibariki Tanzania.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza kwa hotuba yangu ndefu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Rais wa Zanzibar; Mheshimiwa Jaji Mkuu; Waheshimiwa Rais Wastaafu au labda Rais Mwinyi angependa nisema Marais Wastaafu:-

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima kubwa na unyenyekevu sana namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano atoe neno la shukrani, *a vote of thanks. (Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waheshimiwa Marais wastaafu; Mheshimiwa Jaji Mkuu; Mheshimiwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Waheshimiwa Wabunge:-

Nimesimama hapa ili kwa niaba yenu nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake iliyochukua zaidi ya saa mbili. Kabla sijatoa shukrani hizo naomba mniruhusu niseme kwamba nina hakika nitakuwa ninasema maoni ya Wabunge waliokaa humu ndani kwamba tunajisikia wa faraja sana sisi Watanzania tunapowaona Marais wetu Wastaafu wa Awamu ya Pili na wa Awamu ya Tatu wanakuwepo Bungeni kumwona Rais wa Awamu ya Nne akizindua Bunge. *(Makofi)*

Sisi ni nchi pekee nadhani Afrika wenye utamaduni wa namna hiyo. Tunawashukuru Marais hawa kwa kutuwekea misingi hii ambayo Rais wa Awamu ya Nne ameahidi kuyaendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata kwenye uchaguzi tarehe 14 Desemba, mwaka huu 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushindi huo ni uthibitisho kuwa wananchi wana imani kubwa kwake na kwa Chama cha Mapinduzi. Naomba niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge wote walioshinda na kuwepo humu ndani. Nakupongeza na wewe Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa na Wabunge hawa, kuwa Spika wa Bunge letu, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami niruhusu kwa unyenyekevu mkubwa na kwa heshima na taadhima kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri Mkuu na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunidhibitisha kuwa Waziri Mkuu. Mmenipa kura nyingi sana, nawashukuru sana hata wale wawili ambao hawakunipa kura nawashukuru pia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzito na iliyosheheni maelezo ya kazi na majukumu yanayoikabili Serikali ya Awamu ya Nne. Katika hotuba hiyo Mheshimiwa Rais ameeleza vilevile mikakati mbalimbali ya kiutendaji na kiutekelezaji ambayo itahakikisha kuwa tunakusanya nguvu za Wadau wote wa maendeleo ya Taifa letu na raslimali zetu na kuelekeza katika kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu ni mtu muungwana sana, sote tumemsikia akiwashukuru wale wote waliofanikisha mchakato wote wa uchaguzi wetu

mkuu na vilevile amewashukuru wananchi tangu siku aliyoapishwa na kila alipopata fursa ya kukutana na makundi mbalimbali alifanya hivyo kwa jamii nzima. *(Makofi)*

Lakini udhibitisho mkubwa wa uungwana wake ni ahadi aliyoitoa kuwa atawatumikia wananchi wote kwa uwezo wake wote na kutimiza matumaini makubwa waliyonayo kwake na kwa Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Bunge lako Tukufu kuwa sisi tuliopewa na wale watakaopewa heshima ya kuwa wasaidizi wake wa karibu tutatekeleza majukumu yetu kwa umakini na umahiri mkubwa ili kumwezesha kutimiza ahadi yake hiyo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais amebainisha majukumu ya Serikali ya Awamu ya Nne. Sihitaji kuyapitia maana naamini kwamba wakati wa Bunge lijalo katika Mkutano wa Pili tutapata nafasi ya kuipitia hotuba hiyo na kujadili kipengele baada ya kipengele. *(Makofi)*

Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa mkweli kuhusu hali ya siasa katika nchi yetu. Ninategemea kwamba ujasiri huo utajitokeza vilevile kwa viongozi wengine ndani ya nchi yetu katika kuhakikisha amani na utulivu vinakuwepo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais amesisitiza sana suala la mazingira. Sisi wote ni mashahidi, kwa hiyo, naamini tutachukua hatua zinazopasa kwa wakati muafaka ili kuhakikisha kwamba hali ya mazingira haiendelei kuharibika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisimama kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini kama nilivyosema tutapata nafasi ya kuijadili hobuta hii katika kipindi cha Mkutano wa Pili wa Bunge hili, nisiseme mengi. Napenda kurudia kumpongeza sana kwa hotuba nzuri na mimi naamini kwamba kwa maelezo haya, Chama cha Mapinduzi kitatekeleza ahadi zake kwa wananchi wetu na kwa hakika Tanzania yenye neema itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Rais wa Zanzibar; Mheshimiwa Jaji Mkuu; Marais wastaafu; Waheshimiwa Wabunge; sasa ni wakati mzuri wa kuweza kusitisha shughuli zetu ili pale nje tufanye mambo miwili.

Kwanza, ni kupumua tu baada ya maneno kama haya mazito sana, lakini pili tuweze kupiga picha.

Kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge kwa kipindi kifupi. Baadaye kengele itapigwa ili tuweze kurejea na kumaliza shughuli za Bunge. Nakumbushwa na

Mheshimiwa Rais kwamba Wabunge wote mmealikwa Chamwino jioni mara baada ya kumaliza shughuli zetu hapa za Bunge. *(Makofi)*

*(Saa 12:11 Jioni Bunge Lilifungwa kwa Muda Mfupi ili Kupata Fursa ya Kupiga Picha ya Pamoja na Rais)*

*(Saa 12.45 Jioni Bunge Lilirudia)*

**UCHAGUZI WA WAJUMBE KATIKA BUNGE LA AFRIKA**

**KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wabunge katika Bunge la Afrika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyotangaza awali hatua tunayoingia sasa ni ya kuchagua Waheshimiwa Wabunge wale watano wa Bunge la Afrika. Sasa utaratibu una makundi na kadhalika. Ningeomba sasa Katibu wa Bunge aweze kutuingiza katika zoezi la kupiga kura kwa kutoa maelezo ya awali yanayohusiana na makundi hayo mbalimbali.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, jana tulitoa maelezo kwamba nafasi tano ambazo Tanzania inapaswa kuwa na Waheshimiwa Wabunge katika Bunge la Afrika ziko wazi na kwamba Bunge lifanye uchaguzi ili kupata Waheshimiwa Wabunge watano. Jana ilikuwa ni siku ya uteuzi, nilitoa tangazo hilo kwa Waheshimiwa Wabunge wote na kutoa viandishi ambavyo vinaelekeza taratibu zinazopaswa kufuatwa na kwamba ambao wangependa kuchaguliwa kuwa Waheshimiwa Wabunge watakaowakilisha Bunge letu katika Bunge la Afrika watafute wadhamini na kwamba fomu hizo ziwe zimerudishwa itakapofika saa 10.00. Waheshimiwa Wabunge 10 walichukua fomu hizo. Waliorudisha fomu mpaka saa 10.00 walikuwa ni Waheshimiwa Wabunge saba. Nao ni hawa wafuatao:-

Yapo makundi. Kundi “A” lina Waheshimiwa Wabunge Wanawake. Katika kundi hili amerudisha fomu Mheshimiwa Mbunge mmoja naye ni Mheshimiwa Dr. Getrude Ibengwe Mongella. Hapa tunapaswa Waheshimiwa Wabunge kumpigia kura ya ndiyo au hapana. *(Makofi)*

Kundi la “B” ni Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar. Katika kundi hili anatakiwa Mheshimiwa Mbunge mmoja kutoka Zanzibar achaguliwe kuwakilisha kundi hili. Aliyerudisha fomu ni mgombea mmoja naye ni Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee. *(Makofi)*

Kundi la “C”, Waheshimiwa Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani. Katika kundi hili anatakiwa achaguliwe Mheshimiwa Mbunge mmoja. Waliorudisha fomu ni wagombea watatu na kwa kuwa anatakiwa Mheshimiwa Mbunge mmoja ,Waheshimiwa Wabunge hao watapigiwa kura kumchagua mgombea mmoja kuwakilisha Kambi ya Upinzani katika wagombea hao watatu. Waliorudisha fomu ni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Fatma Maghimbi na Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye. *(Makofi)*

Hivyo basi, Waheshimiwa Wabunge watapiga kura kumchagua mgombea mmoja kwa kuweka alama ya “V”.

Mheshimiwa Spika, kundi la “D”. Katika kundi hili wanatakiwa wachaguliwe Waheshimiwa Wabunge wawili. Waliorudisha fomu ni wawili ambao ni Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe. Hivyo hawa nao wanapaswa wapigiwe kura ya ndiyo au hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya tisa, hawa wanapaswa wajieleze mbele ya Kikao hiki na watumie lugha ya Kiingereza kwa sababu...

**SPIKA:** *Order in the House.*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge utaratibu unaosomwa sasa na Katibu wa Bunge ndiyo unatakiwa uheshimiwe kwa sababu ndiyo uliopo katika *The Pan African Parliamentary Election Rules.* Hatuna njia ya mkato wala hatuna uwezo wa kubadili. Kwa hiyo, tungechukua muda mfupi zaidi kwa kuupitia utaratibu huu kama ulivyo humu. Vinginevyo tutakuwa tunajaribu kufanya kitu ambacho ni batili. Katibu wa Bunge endelea. *(Makofi)*

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuheshimu utaratibu huo kadri utakavyoona ni kwamba kila mmoja wa Wagombea hao atapewa muda ambao utapendekeza na kuona kwamba unafaa na baada ya kujieleza ataulizwa maswali na kuyajibu. Baada ya hapo tutagawa karatasi za kupigia kura. Kura hizo zitahesabiwa na baada ya hapo matokeo tutayaleta kwako Mheshimiwa Spika nayo yatatangazwa rasmi, kura walizopata kwa kila mgombea. Hapa ni mwisho wa maelezo haya.

**MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika Mheshimiwa Akukweti.

**MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako tulipoweka hizi Kanuni mwaka ule za namna ya kuwapata wagombea hawa tulizingatia mantiki kwamba katika Bunge lile Kiswahili hakizungumzwi. Lakini baadaye kukawa na *development* kwamba Kiswahili kimeruhusiwa. Sasa mimi kwa heshima ya lugha yetu na kuitendea haki lugha yetu ningeomba kutoa hoja kwamba hiyo Kanuni ya lazima kuongea Kiingereza itenguliwe na ulazima wa kupiga kura ya “Ndiyo” au “Hapana” pia nao utenguliwe ili wale wapite bila kupingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, Bunge linaruhusu Wagombea wajieleze pia kwa Kiswahili wakipenda.

Pili, kwa wale ambao hawana mpinzani tusiingie katika utaratibu mzima wa maelezo na kupiga kura na kadhalika. Ila nitawaomba kwa heshima ya Bunge Zima na kwa sababu tupo wengine hatujafahamiana vizuri, basi hata wao wafanye kusimama walipo Waheshimiwa Wabunge wenzao wawaone. Nadhani waje mbele maana yake sio rahisi kuwaangalia kwa nyuma, itakuwa haipendezi. Basi, wao waje hapa mbele.

Katibu wa Bunge atawaita kwa majina wale ambao hakuna haja ya kuwapigia kura kwa maana ya kwamba wamepitishwa, basi waje hapa kwa kujitambulisha tu majina. Halafu itachukuliwa kwamba tumekwishamaliza. Itabaki kupiga kura kwa wale wa *group* la "C" ambao Mheshimiwa ni Phares Kashemeza Kabuye, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto wao watajieleza na kutakuwa na fursa ya kuwauliza maswali. Halafu ndiyo tutapiga kura. Muite Mgombea anayetangulia.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Dr. Getrude Ibengwe Mongella.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getrude Mongella unaweza kusalimia Waheshimiwa Wabunge wenzio.

***HON. DR. GETRUDE IBENGWE MONGELLA:*** *Your Excellency Honourable Speaker of the House of the Republic of Tanzania; Hon*ourable *Members of this House. I just want to introduce myself as Dr. Getrude Ibengwe Mongella, the current President of the Pan African Parliament. And I seek for your re-election. Thank you very much. (Applause)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**KATIBU BUNGE:** Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee unaweza kusalimia Waheshimiwa Wabunge wenzako

**MHE. OMAR YUSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wenzangu Asalam Aleykum. Mimi niliyepo mbele yenu kwa jina naitwa Omar Yusuf Mzee, natoka katika Jimbo la Kiembesamaki CCM na ninaamini kwamba kuniteua kwenu kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika hamtajuta. Bado nitaendelea kama alivyosema Mheshimiwa Spika, nitakuwa ni mmoja wa wale ambao wanakwenda na *speed* na ari mpya. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Katibu wa Bunge, wale wawili wengine *Mainland Candidates.*

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Athumani Janguo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Athumani Janguo karibu utusalimie.

**MHE. ATHUMANI M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuweza kuchaguliwa kuwa Spika na ninakuombea Mwenyezi Mungu akuongoze ili Bunge hili uliendeshe vizuri. *(Makofi)*

Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake na kuchaguliwa na Bunge hili na ninaamini kwamba kama kiongozi wa upande wa Serikali atatuongoza vizuri na Mwenyezi Mungu amsaidie katika kazi zake. *(Makofi)*

Tatu, ningeomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupita katika uchaguzi uliopita na ninaamini kabisa kwamba tutaisaidia nchi hii kwa kuweza kutoa ushauri na kupitisha Sheria kama tunavyotakiwa na wajibu katika Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninasema mimi ni Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe na hiki ni kipindi changu cha tatu. Nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa imani ambayo mmeweka kwangu ya kutaka kuniendeleza niendelee kuwa tena Mbunge wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Spika, si kwamba sijui Kiingereza, lakini kwa kuienzi lugha ya Kiswahili nimeamua niseme haya kwa Kiswahili. Nawashukuruni sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, karibu utusalimie.

***HON. PROF. JUMANNE MAGHEMBE:*** *Honourable Speaker; your right Honourable Prime Minister; Honourable Members of Parliament;, Ladies and Gentleman:- I am a Professor Jumanne Abdallah Maghembe, Member of Parliament from Mwanga. I stand before you to express my appreciation for you electing me to become your representative in the Pan African Parliament. Thank you so much. (Applause)*

*Honourable Speaker, before I move out of here I like to congratulate you personally for being elected into the position of Speaker. We have all in a very short time appreciated your running and management of Parliamentary affairs in your motto of standards and speed. Thank you very much. (Applause)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kufikia hapo tunaye kwanza Mheshimiwa Dr. Getrude Ibengwe Mongella ambaye amekubalika katika kundi la Wanawake kama mgombea pekee na kwa hiyo, amepitishwa. *(Makofi)*

Katika kundi la "B" Tanzania Zanzibar Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee naye amepitishwa. *(Makofi)*

Katika kundi la Tanzania Bara Mheshimiwa Athumani M. Janguo na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe nao wamepitishwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, sasa kazi iliyobaki ni kumpata mmoja miongoni mwa watatu kutoka kundi la Vyama vya Upinzani. Kwa hiyo, Katibu wa Bunge utupeleke sasa kwenye upigaji kura ili tumpate huyo mmoja. Basi tuuchukue utaratibu tuwaone, wajieleze kwa kuita mmoja mmoja.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nimeombwa kwamba ile *mic* tuliyokuwa tunaitumia pale tumeihamisha kwa shughuli nyingine na tuombe kwa ruhusa yako wajieleze pale walipo. Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye unapewa dakika zisizozidi tatu kujieleza na baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge wana nafasi ya kukuuliza maswali yasiyozidi matatu kama yapo. Kwa hiyo, karibu sasa ujieleze.

**MHE. PHARES KASHEMEZA KABUYE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge........

**MHE. WILLIAM SHELLUKINDO:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. WILLIAM SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, anayejieleza pale inaelekea wenzake wapo ndani, nadhani ni vyema wangetoka nje wasimsikilize.

**SPIKA:** Ni sawasawa. Nitawaomba sasa Mheshimiwa Fatma Maghimbi na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto watupishe kwanza. Mheshimiwa William Shellukindo ahsante sana kwa hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phares Kabuye unaweza kuendelea sasa.

**MHE. PHARES KASHEMEZA KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika; Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wenzangu; mabibi na mabwana: Aliyesimama hapa mbele yenu ndiye yule mnayemfahamu ndugu yenu Phares Kashemeza Kabuye ambaye ametumwa na Watanzania wanaoishi Katika Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa tiketi ya Chama cha TLP. *(Makofi)*

Nimesimama mbele yenu kuwaomba mnipe rukhsa ya kwenda kwenye Bunge la *Pan African.* Nawaahidi kwamba mimi nikifika kule Afrika itatikisika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kura yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kura yako na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge mabibi na mabwana kwa heshima na taadhima naomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kuna swali moja.

***HON. CHACHA ZAKAYO WANGWE:*** *Honourable Speaker thank you. I would like to ask him a question in English because ......*

*Honourable Speaker the conditions for joining......*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa faida ya wenzetu ambao bado ni wageni humu, Spika akisimama huwezi kusimama tena lazima ukae chini. *(Makofi)*

Sasa la pili, Waheshimiwa Wabunge nakusihini sana suala hili lisituchukue muda mrefu tuwe watulivu na tuwasikilize wenzetu. Mheshimiwa Mbunge akitaka kuuliza swali kwa lugha yoyote, basi tumruhusu kwa sababu ndiyo Kanuni zinavyosema, ana Uhuru huo. Kwa hiyo, naendelea kumruhusu na nalinda uchaguzi wake wa kutumia moja ya lugha hizo mbili kwa sababu ndiyo utaratibu. Mheshimiwa Mbunge aendelea. *(Makofi)*

***HON. CHACHA ZAKAYO WANGWE:*** *Thank you Mr. Speaker. I would like to ask the contestant a question because I speak more comfortably in English. Yes.*

*Mr Phares Kabuye, you know very well this is a globalized world and the conditions for joining this Parliament were specified that the Pre-requisite is to be able to speak English and Kiswahili. Now, can you tell me if first of all you are able to speak English and secondly, can you tell me the consequences of electing somebody who unable to speak English and what would be the indignity that your country would suffer in Africa?*

*Lastly, I would like to know if you know any other language other than English and Kiswahili.*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nijibu swali la ndugu yetu kama ifuatavyo:-

Mimi ni Mwalimu wa Shule za Msingi, Shule za Sekondari na Vyuo. Mwaka 1991 Mheshimiwa aliyekuwa Rais wa nchi yetu, Ali Hassan Mwinyi alinituma niiwakilishe Tanzania katika Semina ya *Commonwealth* Uingereza, sikwenda na Mkalimali. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Maneno hayo!

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Baada ya Semina walisema niwafundishe kwa nini Tanzania tunasema tuna demokrasia wakati huo tuna Chama kimoja. Niliwafundisha Wazungu weupe mpaka wakafurahi. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi.

Walinipa zawadi ya *scholarship* kwenda *Oxford University for two weeks.* Kwa hiyo, *don't worry I can speak English. Thank you. (Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Kuna swali?

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phares Kabuye, ahsante sana unaweza kwenda.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *order in the House.*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali kwa Kiingereza ni Mbunge kutoka Chama cha CHEDAMA. Kwa hiyo, kuna utaratibu wa kuketi. Ningemwomba aondoke sasa hivi, nadhani Katibu msaidieni kumwonyesha mahali pa kukaa.

**MBUNGE FULANI:** Hawajuani!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Order in the House na kama wapo wengine ambao hawana uhakika ieleweke kwamba upande wa mkono wangu wa kulia ninako nyosha huku wanakaa pekee kwa sasa hivi na kwa hali ilivyo na kwa uchaguzi ulivyoenda wanakaa Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala CCM. Upande wangu wa kushoto ni mistari kadhaa ambao nadhani Katibu ataelekeza. Lakini kwa ujumla ni upande huu kutazamana na Spika upande wa kushoto ni wenzetu kutoka Vyama vya Upinzani. Kwa hiyo, naomba hiyo tuifuate.

**SPIKA:** Kutakuwa na Semina katika Kikao chetu cha mwezi wa Februari, 2006 kusaidiana kwa mambo yote haya. Lakini ni lazima tutii taratibu toka mwanzo.

Sasa aitwe anayefuata.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, sasa aje Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mbunge kutoka *CUF. (Makofi)*

**SPIKA:** Karibu sana Mheshimiwa Maghimbi. Unazo dakika tatu za kujieleza mbele ya Wabunge hapa na baada ya hapo watakuwa na fursa ambayo wanaweza kuchagua kuitumia ama vinginevyo ya kukuuliza maswali yasiyozidi matatu. Karibu.

**MHE. FATMA MAGHIMBI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi pia naanza kwa kukupongeza wewe pamoja na Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa kwenu kuwapo katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama mbele yenu leo pamoja na Bunge lako Tukufu kuomba kura ya kuingia katika Bunge la Afrika.

Mimi naitwa Fatma Maghimbi, umri wangu ni miaka 60. Nimesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *degree* yangu ya kwanza ya Sheria na nimesoma *degree* yangu ya pili ya Sheria Uingereza. Mimi nasimama mbele yenu kuomba kura zenu kwa sababu nahisi kwamba ninao uwezo wa kwenda kulitumikia Bunge la Afrika. Kwa sababu Bunge hili la Afrika moja katika malengo yake ni kuleta maendeleo katika nchi za Kiafrika zilizo huru na pia kuangalia haki za binadamu. Kwa hiyo, mimi nahisi katika nyanja hizi naweza kulitumikia Bunge hili ambalo pia linataka kuendeleza mambo ya biashara na uwekezaji. Waheshimiwa Wabunge naomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali? Kuna maswali kule.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa anaomba nafasi hii adhimu na kule Zanzibar Chama chake hakiitambui Serikali ya Zanzibar; Je, atawezaje kuiwakilisha Tanzania wakati sehemu moja ya Tanzania haitambui? *(Makofi)*

**MHE. FATMA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Spika, Bunge la Afrika sidhani kama linahusiana na siasa zozote.

**WABUNGE FULANI:** Ahaa !!!!!!!

**SPIKA:** *Order! Order!* Tusikilize majibu jamani tafadhali.

**MHE. FATMA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Spika, mimi ninachosema ni kufikiria maendeleo ya nchi hii hasa katika uwekezaji, haki za binadamu na ndiyo maana nikaomba katika Bunge la Afrika.

**SPIKA:** Swali lingine!

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mimi sijaelewa vizuri, nataka ajibu ndiyo au hapana. Je, unaitambua Serikali ya Zanzibar?

**MHE. FATMA MAGHIMBI:** Siitambui. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Swali hamna. Ahsante Mheshimiwa Maghimbi.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Mgombea wa tatu ni Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, tunaomba aje kujieleza, anatoka CHADEMA.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto unapewa nafasi ya kujieleza isiyozidi dakika tatu. Ukishamaliza Waheshimiwa Wabunge wanayo fursa ambayo wanaweza kuitumia ama wasiitumie ya kukuuliza maswali yasiyozidi matatu. Karibu sana.

**MHE. KABWE ZUBEIR ZITTO:** Ahsante.

*Honourable Speaker; Honourable Members of Parliament: For the sake of honouring the just resolution that the Parliament has passed regarding the use of language, I would like to use a Swahili language to express myself. (Applause)*

Naitwa Zitto Zubeir Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, ninagombea Ubunge kuwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika. Ninaamini Tanzania inahitaji kutuma mtoto wake mwenye uwezo wa kuiwakilisha vizuri. Nina uwezo wa kuiwakilisha nchi yetu vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, mimi ni msomi, mimi ni Mchumi, nimesomea *degree* yangu ya kwanza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nimesomea *degree* yangu ya pili Chuo Kikuu cha Bonn Ujerumani, ni Mchumi wa Biashara ya Kimataifa. Sasa hivi Bara la Afrika lipo kwenye hatua ya kuwa katika *Economic Community.* Biashara ndiyo ambayo itaongoza Bara la Afrika. Ninaamini, nina uwezo wa kufanya hivyo.

Mwisho Waheshimiwa Wabunge, mimi nina uzoefu. Mimi ni *Pan-Africanist* wa muda mrefu. Nimekuwa Katibu Mkuu wa *Pan-African Youth Movement* tawi la Tanzania, nimekuwa niki-*organize* Mikutano ya Siku ya Afrika kila mwaka toka nilipojiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa hiyo, Bara la Afrika na matamanio ya Bara la Afrika kuungana nayajua vizuri. Naomba mnichague. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Zitto.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata sasa hivi ni kuwagawia Waheshimiwa Wabunge karatasi za kupigia kura. Karatasi hii ina majina matatu ya Wagombea, lakini anayetakiwa ni mmoja tu. Kwa hiyo, alama inapashwa kuwekwa baada ya jina la mtu anayependekezwa. Baada ya hapo kama desturi, kura zitakusanywa na kuhesabiwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba masanduku yaje, karatasi za kupigia kura tuwagawie.

Desturi tuliyonayo ni kwamba Wabunge wote ambao ni Wapigakura ni lazima waitwe na kuwepo katika Ukumbi huu kwa kupiga kengele. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani utaratibu huu tuufuate, kengele ipigwe masanduku yaje. *Sorry,* karatasi za kura zigawiwe ili kila mmoja apate kutimiza haki yake.

Ahsante Mheshimiwa Spika.

*(Hapa kengele ilipigwa)*

**SPIKA:** Yafungue masanduku muyaonyeshe kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba hayana karatasi zozote. Yainueni waone Waheshimiwa Wabunge.

*(Hapa masanduku yaliyo wazi yalionyeshwa kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**SPIKA:** Haya, gawa karatasi za kura.

Waheshimiwa Wabunge wote mmepata karatasi?

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Bado.

**SPIKA:** Mbona *slow* namna hii? Jamani harakisheni kugawa karatasi, haina tatizo lolote.

*(Hapa karatasi za kura ziligawiwa kwa Wabunge)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika ........

**SPIKA:** Endelea !!!!!

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nimepata karatasi ya kupiga kura, lakini kwa niliyoipata mimi inaonyesha majina mawili, lakini upande wa Vyama inaonyesha Vyama vyote. Sasa sijui hii kura...

**SPIKA:** Hebu irejeshe kwa Wahudumu tuone. Ina makosa hiyo!

*(Hapa karatasi ya kura ilifunguliwa na kurejeshwa kwa Wahudumu)*

**SPIKA:** Ambaye hajapata karatasi ya kura anyooshe mkono. Nani hajapata karatasi ya kupigia kura? Kwa hiyo, wote tumepata na tumekwishapiga nadhani. Kwa sababu ni *tick* moja tu ambayo inahitajika.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Ndiyo !!!!

**SPIKA:** Basi vijana muanze kukusanya hizo kura zilizopigwa.

*(Hapa karatasi za kura zilikusanywa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Wagombea wanapewa nafasi ya kuteua Mashahidi au Wasimamizi wakati kura zinahesabiwa. Mheshimiwa Kabuye?

**MHE. FARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Suleiman N'hunga. Mheshimiwa N'hunga basi ......

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Maghimbi?

**MHE. FATMA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Spika, wote nawaamini watakaokwenda kuhesabu kura.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto?

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Namteua Mheshimiwa Halima James Mdee.

**SPIKA:** Tamka kwa sauti sikusikia vizuri.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Namteua Mheshimiwa Halima James Mdee.

**SPIKA:** Mheshimiwa N'hunga na Mheshimiwa Halima waje hapa mbele.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa N'hunga ametoka nje.

**SPIKA:** Dharura?

**MBUNGE FULANI:** Kwa maana hiyo hayupo.
**SPIKA:** Mheshimiwa Kabuye teua mwingine, Mheshimiwa N'hunga yupo nje.

**MHE. FARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Ndugai. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana mwenzetu Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya aliuliza swali kuhusu Fomu za Maadili za Uongozi kutoka Tume ya Maadili. Alitaka kujua kwa sababu Uchaguzi uliahirishwa na Waheshimiwa Wabunge wamepatikana baada ya tarehe 14 Desemba na kwa kawaida fomu zile zilikuwa zinatakiwa kurudishwa tarehe 31 Desemba na wengi wamezipata si zaidi ya wiki moja hii iliyopita, wengine jana. Sasa utaratibu uweje?

Tumepata ufafanuzi kutoka Tume ya Maadili. Ni kwamba fomu zile sasa mtatakiwa Waheshimiwa Wabunge mzirejeshe panapohusika kabla ya tarehe 31 Januari, 2006. Nadhani tangazo hili linaondoa utata wowote uliokuwepo kwa sababu mnaweza kutulia mkasheherekea mwaka mpya, baada ya hapo kwa kasi yoyote mliyonayo mkazijaza na kuzirejesha bila ya kuwa na matatizo yoyote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILBROD P. SLAA:** Mwongozo wa Spika......

**SPIKA:** Endelea!!!

**MHE. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia Kanuni ya 55(3) kuomba ufafanuzi kidogo na Mwongozo wa Spika kuhusu jambo lililotokea hapa Bungeni ambalo linahusiana na Kanuni zetu za Bunge la Afrika, Kanuni ya 17.

Mheshimiwa Spika, katika kanuni hii tumefanya *amendment* ya kanuni zetu. Ninaelewa *pressure* tuliyonayo, tatizo kubwa tulilonalo, nafasi ambayo hasa Mgombea wetu ambaye ni Mwenyekiti au Rais wa Bunge la Afrika. Lakini kimsingi, Bunge ni Taasisi inayotunga Sheria, Taasisi inayopaswa kuwa mfano, inayopaswa kuonyesha njia na tulichofanya ni ku-*amend* hizi sheria bila ya kufuata utaratibu ulioko kwenye Kanuni hii. Naomba ninukuu kwa kibali chako. *"These rules may be amended at any time by resolution of the National Assembly on a proposal submitted to it by the Standing Orders Committee".*

Kanuni na Sheria zinapowekwa kwa kawaida zinapenda kulenga, kutunza, kuhifadhi, kulinda taratibu zilizowekwa. Sasa tume-*amend* hapa. Ninaelewa tatizo, inawezekana sina ugomvi, lakini ningependa kulinda heshima ya Bunge letu huko mbele na nisingependa kuona vitu vya namna hii huko mbele vinafanyika. Sasa ningependa kuona ufafanuzi kutoka kwa Spika kama jambo hili tulilofanya tunaweza kuli-*regularize* namna gani, nadhani ndiyo taratibu za kawaida za sheria.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa hilo. Kwa uamuzi tuliochukua tulikuwa *guided* na Kanuni inayohusu "Kutengua." Katika mfumo wa Mabunge ya *Commonwealth* kuna uwezo ambao umetolewa kwa kila Bunge kuzingatia hali halisi ya wakati, kutengua Kanuni yoyote. Kwa hiyo, mimi nadhani kilichofanyika hivi sasa sio kubadili, tumeziweka kando ili tufuate utaratibu ambao unatuwezesha kufikia lengo na masuala haya unaweza kuyakuta mara kwa mara.

Ningeomba Waheshimiwa Wabunge katika kipindi hiki tunachopitia na hasa ukizingatia kwamba hata Kanuni zetu kwa kiasi kikubwa zimepitwa na wakati, basi Spika huyu anayezungumza nanyi hivi sasa wakati wote ataegemea busara za kawaida kuliko kufuata maandiko mpaka hapo tutakapoweza kubadili hizi Kanuni ili mradi kinachofanyika ni cha maslahi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, uamuzi wetu unasimama pale pale na yote tuliyoyafanya ni sahihi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kutoa taarifa kwa Bunge hili. Suala la Kiswahili kutumika kwenye AU lilikwishakubalika na AU na mtu wa kwanza kusema Kiswahili kwenye Mkutano Mkuu wa AU uliopita alikuwa ni *President* Chissano kutoka Msumbiji. Kwa hiyo, tusitwange maji kwenye kinu. Nimeona nitoe taarifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Malecela kwa hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda uliosalia kwa mujibu wa Kanuni hautoshelezi sisi kuweza kuikamilisha shughuli iliyoko mbele yetu katika wakati,

ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe hoja au Mwanasheria Mkuu atoe hoja ili tuweze kuendelea nje ya wakati ambao umo katika Kanuni hadi tumalize shughuli iliyosalia. *(Makofi)*

**HOJA YA KUONGEZA MUDA WA BUNGE KUKAA**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 21 fasili 4 ya Kanuni za Bunge, kwamba Bunge liruhusu kuongeza muda wa kikao ili tuweze kukamilisha Shughuli za Uchaguzi wa Wagombea wa nafasi za Uwakilishi katika *Pan African Parliament*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. PHILLEMON SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kuongeza Muda wa Bunge ili Kumaliza Kazi ya Uchaguzi iliyopo Mbele ya Bunge)*

**SPIKA:** Kwa muda huu nataka nimruhusu Katibu wa Bunge atoe matangazo ya Kiutawala.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nina matangazo mawili. La kwanza ni kuhusu *Sitting Allowance*. Tumechelewa kidogo kushughulikia suala hili kwa sababu bado tulikuwa hatujapata utaratibu rasmi ambao tunautumia wa ukaaji ndani ya Ukumbi huu.

Lakini tumetumia orodha ya majina ambayo tumeipata kwa Wabunge wote ambao wamekula kiapo cha Uaminifu na kwamba tayari tumekamilisha kazi hiyo na kwa hiyo malipo kwa ajili ya *Sitting Allowance* yapo tayari.

Tangazo la pili, linahusu usafiri wa kwenda Chamwino. Mabasi yatakuwa tayari baada ya kumaliza shughuli zetu hapa kwa ajili ya kutupeleka sote Chamwino na kurudi hapa.

Mwisho wa matangazo ya kiutawala. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimepokea rai hapa ya baadhi ya wenzetu ambao wangependa kwa kauli zao wenyewe kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nilidhani badala ya kukaa tu hatufanyi kitu chochote, hili nalo ni jema kwa Bunge. Kwa

hiyo, wale ambao wako tayari sasa nitaomba wasimame kama ulivyo utaratibu halafu nitamtambua.

**MHE. WILLBROAD P. SILAA:** Mheshimiwa Spika, noamba kwanza nikushukuru kwa kukubali rai hiyo kuliko kutazamana. Ni vyema kweli tukatumia nafasi katika kupongezana, nadhani ndiyo raha ya Bunge lenyewe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia nafasi hii, kwanza kabisa kukupa pongezi wewe mwenyewe kwa kuteuliwa, kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge letu na ningependa kutumia nafasi hii hiyo hiyo kukupongeza kwa mabadiliko ya haraka sana yaliyokuja kwa *speed* kubwa sana ambayo yameonyesha uhai mpya wa Bunge letu. *(Makofi)*

Mabadiliko tuliyoyaona kwa muda mfupi ni makubwa sana, yanatupa imani kwamba kazi yetu katika Bunge hili itakuwa rahisi na itakuwa ya ushirikishwaji kama ulivyoanza na tunakutakia Mwenyezi Mungu akupe nguvu ili uweze kufanya kazi hiyo vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye ameshinda kwa kura nyingi kutokana na uchaguzi wa tarehe 14. Lakini napenda kumpongeza kwa dhati pia kwa hotuba yake aliyotoa mchana huu ambayo imetoa dira ya utekelezaji wa mpango wetu wa kazi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Ni imani yangu kwamba kama Rais alivyosema Bunge letu litachukua msimamo huo kwamba tutafanya kazi kwa ushirikiano na mshikamano kwa sababu lengo letu wote ni moja, kuitumikia Tanzania na kutumikia Watanzania. Ndani ya Bunge tunaamini kwa kawaida ushabiki unakuwa pembeni kwa sababu maslahi ya Taifa ni makubwa kuliko ushabiki. *(Makofi)*

Lakini napenda kumpongeza vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu, Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na pia kwa kuthibitishwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu. Kama nilivyosema, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Lowassa ni jirani yangu pale Arusha, lakini ni Mwenyekiti wangu wa Wabunge wa Arusha, sina hakika kama sasa atanikimbia na mimi ni Katibu wake, kwa hiyo, ninafahamu utendaji kazi wake, ninafahamu uchapaji kazi wake, ninafahamu jinsi anavyoipenda nchi hii na kwa msingi huo ningependa kumwombea neema tele kwa Mwenyezi Mungu aweze kufanya kazi hii kwa hekima kubwa na baraka za Mwenyezi Mungu na aweze kuwasaidia Watanzania katika ujumla wao kwa sababu wanahitaji viongozi ambao kwa kweli ni wachapakazi katika kipindi hiki tunachokiendea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nilitaka kusema tu nakushukuru kwa kunipa nafasi hii tuliyoipata tuitumie wakati tunangojea matokeo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya *United Democratic Party,* nikiwa ni miongoni mwa baadhi ya viongozi wa nchi hii waliopo ndani ya Bunge hili, nataka kutumia nafasi hii kwanza

kabisa kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwa kishindo, sio tu kwa Bunge hili lakini hata pia kwenye Jimbo lako. *(Makofi)*

Nataka kuungana na mwenzagu kutoka CHADEMA aliyesema kweli uliyoyasema katika ufanyaji wako wa kazi *speed* ndiyo itakuwa msimamo wako, ni kweli imeonyesha kuna mambo tayari umeshayapeleka kwa *speed* kubwa sana katika Bunge hili na hii inaendana na kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya na sisi tukiwa baadhi yetu wazee wa nchi hii, tunafurahi kwamba tumeletwa na wananchi ili kuhakikisha hiyo kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya inakuwa *properly tested* na inakwenda ikiwa na *break* pia. Maana ikienda bila *break* inaweza ikaleta madhara makubwa sana katika Taifa hili. *(Makofi/ Kicheko)*

Kwa hiyo, naomba niachane na hilo, nitumie nafasi hii kukupongeza sana. Sisi katika UDP tuna imani sana na wewe na tunamwomba Mwenyezi Mungu akubariki, akupe busara na pia akupe uzima. Unajua kukaa hapo ni kazi kubwa sana, lakini sisi tuna imani kwa sababu wewe mwenyewe umeiwakilisha Tanzania ukiwa unaongoza kitengo cha *Tanzania Investment Centre.* Kama kijana wangu hapa alivyosema, tunakokwenda uchumi ndiyo litakuwa jambo ambalo ni la maana na biashara katika miaka hii mitano inayokuja. Kwa hiyo, kwa kuwa unajua sana mambo ya uwekezaji ninahakika Bunge hili litatumika vizuri sana katika kuhakikisha kwamba tunapata *investment* nzuri zaidi kwa ajili ya Taifa hili.

Pili, umeonyesha wazi kwamba wewe ni mtu ambaye utatutumikia sisi wote kwa haki na leo umeonyesha kitu kipya. Jana ulionyesha kitu kipya cha vazi la Naibu Spika na leo umeonyesha kitu kipya cha mawazo kwamba Kanuni zipo hapa kwa ajili ya kutusaidia, lakini utatumia zaidi hisia na hali halisi katika kuongoza shughuli za Bunge hili.

Mimi nafikiri Kambi yetu ya Upinzani kazi yake ni kukusaidia wewe na Bunge hili ili liweze likafanya maamuzi yaliyo bora kwa ajili ya wananchi wetu wote na mimi nina hakika walio wengi ni wakulima. Mimi ningefikiri katika miaka mitano wakulima watapata sauti kubwa sana katika Taifa hili na mimi naweza kukuhakikishia tangu mwanzo hoja yangu itakuwa pamba. Kwa hiyo, haya mambo nafikiri wewe na uzoefu wako wa kutukutanisha pamoja utatusaidia sana katika kufanya maamuzi.

Pia, nataka kuwepo na amani katika Bunge hili, najua tuko Vyama mbalimbali, lakini wote tupeane nafasi ya kuweza kutoa mawazo yetu kwa hali ya amani na utulivu kwa sababu lengo letu ni moja kwa wananchi wa Tanzania.

Nikimalizia hapo, nataka kutumia nafasi hii pia kuungana na wenzangu wa CHADEMA kwamba Rais leo naye ametuonyesha kitu kipya. Kwa mara ya kwanza hatujaona Rais anazungumza kwa masaa mawili bila kusoma. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo ningependa kulipongeza sana. Watu wote tuliokuwemo mule tuliona kama tunazungumza na mtu *rather than* kupata hotuba ambayo labda imeandaliwa na mtu fulani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka kumpongeza Rais kwanza kwa kuchaguliwa na sisi kule tulimpa kura nyingi sana, kwa hiyo hatuna tatizo na hilo na pia ameonyesha kweli yupo tayari kuunganisha watu wa aina mbali mbali kwa mikakati ambayo ametupa hapa. Tutafute vitu vinavyotuunganisha Watanzania zaidi kuliko kutafuta vitu vinavyotutenganisha. Hili ni jambo ambalo ni la maana.

Mwisho, nataka kutumia nafasi hii kumpongeza sana rafiki yangu Edward Lowassa, lakini sio tu kwamba nampongeza kwa sababu ni rafiki yangu, nampongeza zaidi kwa sababu miaka mitano ambapo amekuwa Waziri wa Maji na Mifugo tumeona wazi wazi umahiri wake katika kufuatilia mambo na sisi zaidi watu wa Shinyanga tunashukuru sana kwamba tumepata maji Shinyanga na mradi unafaanya kazi. Kwa hiyo, ametumia ule uzoefu wa wale waliokuwepo zamani kuhakikisha hili jambo linatekelezeka.

Kwa hiyo, mimi natoa mkono wangu wa ushirikiano wa Chama chetu, tuko tayari kushirikiana kwa yale yote mazuri ambayo yatakayoweza kusaidia Taifa letu. Tuna imani na wewe utafanya kazi na Mwenyezi Mungu akubariki.

Baada ya kusema hayo, sisemi kwamba kila kitu tutakubaliana naye, lakini kutokukubaliana kusiwe msingi wa kutokuwa marafiki au Watanzania. Tuko hapa ili tuweke mambo yetu sawa kuboresha maamuzi ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kutumia nafasi hii kumpongeza Naibu Spika, ambaye pia jana amechaguliwa, asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimekwishamkubalia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, kwa hiyo, ingawa matokeo yako tayari, ningeomba uvumilivu wenu kwa dakika mbili tumruhusu Hamad Rashid Mohammed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, nitachukua dakika mbili tu kwa sababu najua tunakimbilia kwenda Chamwino.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kukushukuru na kukupongeza, lakini pia nimpongeze Naibu Spika, ambaye nimewahi kufanya naye kazi mwaka 1978 nikiwa Mbunge na yeye akiwa kwenye Kamati ya *Public Accounts Committee* pamoja na mimi namfahamu sana utendaji wake na ninaamini Bunge limepata viongozi shupavu na nafikiri tutakwenda kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili na mimi nimpongeze Rais kwa hotuba yake, Rais amegusa mambo ya msingi na hasa alilogusa ni suala zima la amani na utulivu katika nchi yetu na kwamba tuondokane na migogoro ambayo itarudisha nyuma maendeleao ya nchi yetu na hasa pale aliposema kwamba ameguswa sana na suala la Zanzibar na akaomba kwa kweli viongozi wote tushirikiane pamoja katika kupata ufumbuzi.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba Bunge hili tutakuwa tayari kutoa kila msaada katika kila hali kuhakikisha migogoro hii inamalizika ili tupate nafasi ya kujenga nchi yetu. Sisi Watanzania tumekuwa mstari wa mbele kutatua migogoro ya nchi mbalimbali. Ni aibu leo Rais wetu akitoka nje ya nchi akaulizwa kuwa ndani ya nchi yako kuna mgogoro. Nguvu yake itakuwa ndogo sana! Tunahitaji kumsaidia na tunamhakikishia tutampa msaada wetu wa hali na mali ili kufanikisha hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, rafiki yangu na mimi sana, tumefanya kazi pamoja, mimi naingia Bungeni 1978 walipokuwa wao mwaka 1980 tukawapokea vizuri tu. Kwa hiyo, tunafahamiana sana. Naomba kumhakikishia kabisa atapata msaada wote anaohitaji, tutatoa ushirikiano wa kila hali, lakini ajue tu kwamba Kambi ya Upinzi ni *check and balance* katika *Parliament.* Tunapofanya hivyo tutafanya kwa uadilifu, kwa uaminifu, tukielewa kwamba tunahitaji kutoa mashirikiano na kuisaidia Serikali kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijatangaza haya matokeo, nilitaka kueleza kwamba kwa masikitiko, wakati Rais anaongea hapa, kuna simu za mkononi mbili za Wabunge zilitoa milio. Sio jambo zuri na kwa kweli hairuhusiwi kabisa kuwa na simu ya mkononi ikipigapiga kelele humu wakati tunaendele na shughuri za Bunge. Nilipata bahati leo asubuhi, nilikwenda kumsalimia mzee wangu, Mheshimiwa John Samweli Malecela, katika mambo mengine tuliyozungumza akanieleza kwamba katika Bunge la Zambia Mbunge anaingia na simu na akiiacha wazi na ikaita, adhabu yake ni kwamba Spika anamwita *Sergeant At Arms* na simu ile inataifishwa.

Sasa najua sisi tuko katika awamu za ubinafsishaji zaidi na sio utaifishaji. Lakini pengine nitaongea na Mwanasheia Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu ili na sisi tuone. Haya ni mambo ya aibu kabisa yanapotokea na unajua ni rahisi sana kusahau. Kwa hiyo, tutatafuta ufumbuzi, tutashirikisha Waheshimiwa Wabunge na Kamati mbalimbali, lakini kweli ni aibu kabisa Rais wetu anaongea hapa Mheshimiwa anahangaika na simu inaita inakuwa sio vizuri. *(Makofi)*

## MATOKEO YA KURA ZA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA

**SPIKA:** Baada ya hapo matokeo ya kura tulizopiga kuwapata wenzetu watano kwa Bunge la Afrika ni kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge waliopiga kura walikuwa ni 314, kura zilizoharibika ni tatu. Kwa hiyo, idadi ya kura halali zilizopigwa ni 311.

Matokeo: Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto amepata kura 27, Mheshimiwa Fatma Maghimbi amepata kura 31 na Mheshimiwa Fales Kashemeza Kabuye amaepata kura 253. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namtangaza Mheshimiwa Kabuye kuwa ndiye mshindi na ndiye mwakilishi wetu katika kundi la Vyama vya Upinzani. Ni mwakilishi Mbunge kuingia katika Bunge la Afrika na kwa maana hiyo, sasa natangaza rasmi, sasa wenzetu hawa watano akina nani?

Waheshimiwa Wabunge, tuliowachagua katika Bunge hili kuwa Wabunge katika Bunge la Afrika ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Dr. Getrude Mongella, halafu Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mheshimiwa Athuman Janguo na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe. *(Makofi)*

Hapo ndiyo mwisho wa uchaguzi wetu na nadhani ndiyo tumefikia mwisho wa shughuri zetu. Ila tu sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe hoja ya kuahirisha Bunge. Katibu.

**KATIBU WA BUNGE - (DAMIAN. S. FOKA):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kufanyiwa kazi katika Mkutano wake wa Kwanza katika Bunge hili jipya sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, toa hoja ya kuahirisha Bunge.

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, leo tumepongezana vya kutosha. Kwa hiyo, mniruhusu nisiendelee kupongeza, lakini nikupongeze kwa kuongoza Kikao hiki cha jioni na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuingia Bunge la Afrika, nawapongeza sana.

Nawapongeza vilevile Mheshiwa Willbroad Slaa, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed kwa hotuba zao walizotoa leo hii jioni. Nawashukuru sana, tunawashukuru kwa kutuhakikishia kwamba tutafanya mashirikiano ili tufanye kazi za nchi yetu kwa faida ya maendeleo ya watu wetu. Tunawashukuru sana.

Nawashukuru pia kwa kumpongeza Rais, tutamfikishia salaam hizo lakini tuna nafasi ya kuchambua hotuba hiyo kama nilivyosema wakati wa Kikao kijacho. Kwa hiyo, nina hakika tutapata nafasi ya kuchambua zaidi lakini kwa sasa nawashukuru kwa pongezi mlizompa Mheshimiwa Rais na tutamfikishia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwisho, naomba niwatakieni safari njema na niwatakieni sikukuu njema ya mwaka mpya. Naamani baada ya kazi ndefu ya uchaguzi na safari hii bila shaka mtapata nafasi ya kupumzika vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako liahirishwe hadi tarehe 7 Februari, 2006 saa tatu asubuhi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. M. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naliahirisha Bunge hili hadi siku ya jumanne tarehe 7 Februari, 2006 hapa Dodoma saa Tatu asubuhi na kheri za mwaka mpya. *(Makofi)*

*(Saa 02.07 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne*
*Tarehe 07 Februari, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*